Mwongozo Wa Mwalimu

7

# Kanuni za Kikristo

## Zinazohusiana na kanisa la mahali pamoja na kanuni zake



MVMM

Mafunzo ya Vikundi Yanayohusu Maisha Mapya

# Kanuni za Kikristo

## Zinazohusiana na kanisa la mahali pamoja na kanuni zake

Kimeandikwa Na David Batty

Mwongozo Wa Mwalimu

Toleo la Tano

Mafunzo ya Vikundi Yanayohusu Maisha Mapya

# Kanuni za Kikristo

## Zinazohusiana na kanisa la mahali pamoja na kanuni zake

Kimeandikwa Na David Batty

Mwongozo Wa Mwalimu

Toleo la tano

Maandiko Yanayotumiwa Katika Kitabu Hiki Yametoka Kwa:

MAANDIKO: Biblia Takatifu (Union Version). Toleo La 1952, 1974, 1976, 1978. BST, BSK. Yametumiwa Kwa Ruhusa Maalum.

Tafsiri Ya Lugha Rahisi (TLR) itakayofanywa na mtafsiri ili kuleta maana halisi kama inavyosomeka katika lugha ya Kiingereza.

HakiMiliki © 2023, Teen Challenge USA.

Vitabu vya Mwalimu na kila kitu cha mwanafunzi vinavyohusiana na masomo haya ya *Mafunzo ya Vikundi Yanayohusu Maisha Mapya* vinanatawaliwa na Sheria za HakiMiliki. Mpango maalum umefanywa ili kufasiri masomo haya kwa lugha hii yaKiswahili. Masomo haya yanaweza kuchapwa na kugawanywa kwa ajili ya matumizi katika huduma za Teen Challenge na zinazofanana nazo, katika makanisa ya mahali pamoja, shule na mashirika mengine na hata watu binafsi. Pia, yanaweza kupatikana kutoka kwa mtandao kwenye tovuti hii: www.iTeenChallenge.org Lakini, yasiuzwe. Yatolewe bure. Kwa wanaotaka kuchapisha na kuuza, wapate ruhusa kwa maandishi kutoka kwa Global Teen Challenge.

Kwa mara ya kwanza, somo hili lilichapishwa kwa Kiingereza kwa jina lifuatalo: *Christian Practices, 5th edition*

Somo hili ni sehemu ya mfululizo wa masomo yaitwayo *Mafunzo ya Vikundi Yanayohusu Maisha Mapya* yanatawaliwa ili kutumiwa makanisani, shuleni, katika huduma za gerezani, huduma za Changamoto Kwa Vijana, na huduma zingine kama hizo zinazofanya kazi na Wakristo Wapya. Vilevile kuna vifaa vingine vinavyopatikana kwa ajili ya mafunzo haya, kama kitabu cha kumwongoza mwalimu, cha kumwongoza mwanafunzi, cha Mwongozo Wa Somo cha mwanafunzi, mtihani, na cheti. Ukitaka habari zaidi juu ya masomo haya, wasiliana na:

Global Teen Challenge
PO Box 511
Columbus, GA, 31902 USA
Barua Pepe:gtc@globaltc.org
Tovuti: www.globaltc.orgna
www.iTeenChallenge.org

MVMM
Mafunzo ya Vikundi Yanayohusu Maisha Mapya

Mwaka wa Mwisho Kuhakikiwa: 12-2023

# Kanuni za Kikristo

Kozi hii inaangazia mada sita zinazohusiana na kanisa la mahali pampja. Lengo kuu ni kuonyesha jinsi Wakristo wapya wanavyoweza kushirikiana pamoja kwa njia yenye maana na Wakristo wengine katika kanisa lililo kwenye jamii yao.

**1**

### Sura 1. Kanisa la mahali pamoja

Tutajifunza kanisa ni nini na ni kwa nini makanisa yapo. Pia tunaangalia jinsi Mungu anataka makanisa ya mahali pamoja kuhudumia watu katika jamii hiyo.

**2**

### Sura 2. Jinsi ya kutoa ushuhuda

Sura hii inahusisha mjadala kuhusu mambo unayoweza kujumuisha unapowaambia wengine yale Mungu anafanya maishani mwako.

**3**

### Sura 3. Jinsi ya kuwa meneja wa Mungu

Tunajifunza jinsi Wakristo wanavyoweza kutumia vizuri vitu mbalimbali ambavyo wamepewa na Mungu. Sehemu kuu zinazojadiliwa ni wakati wetu, uwezo, na mali za kibinafsi.

**4**

### Sura 4. Ushirika Mtakatifu

Lengo kuu la somo hili ni kuchunguza kusudi la ushirika kwa Wakristo leo.

**5**

### Sura 5. Ubatizo kwa Maji

Tunachunguza ni kwa nini Wakristo wanapaswa kubatizwa kwa maji.
Hoja kuu ya sura hii ni kuweka wazi maana ya kiroho ya ubatizo wa maji.

**6**

### Sura 6. Maombi

Mafunzo haya yanahusu maana ya maombi, na kile kinachopaswa kuwa katika maombi yetu. Pia tunazungumzia jinsi ya kupata majibu ya maombi yetu.

## Yaliyomo Katika Mwongozo Huu Wa Mwalimu

Kitabu hiki kina sehemu nne. Kila sehemu imeanza kwa ukurasa wenye rangi ya njano, ambao ni ukurasa ulio na jina la mada.

1. Mipango Ya Mwalimu ya Kufundishia Somo
2. Mwongozo Wa Mwanafunzi
3. Mwongozo Wa Somo
4. Mtihani Wa Mwanafunzi Na Cheti Cha Somo

Maelezo kuhusu jinsi ya kutumia kila sehemu yanapatikana mara tu baada ya utangulizi wa ukurasa unaofuata.

# Utangulizi

Hili ni somo moja katika mfululizo wa masomo ulioandaliwa kwa ajili ya kuwafundisha Wakristo wapya. Tunaamini kwamba lipo hitaji kubwa sana siku hizi la kuwasaidia Wakristo wapya ili wahusishe mafundisho ya Kristo na maisha yao ya kila siku kwa vitendo. Mafundisho haya pia yanaweza kutumiwa vizuri sana kwa ajili ya huduma kwa vijana kanisani na watu wazima wanaotamani kufanya Ukristo kuwa sehemu ya maisha yao kila siku.

Kusudi kubwa la somo hili na mfululizo mzima wa *Mafunzo ya Vikundi Yanayohusu Maisha Mapya* ni kuwatambulisha Wakristo wapya kwa maswali muhimu yanayohusu maisha. Hatujaribu kuwapa mafundisho yatakayokuwa ndiyo mwisho kuhusu mada husika.

Kamati ya Mtaala ya Huduma ya Teen Challenge Marekani, ina mpango wa kuendelea kupitia upya na kufanya marekebisho kwa masomo haya. Tunakaribisha mawazo yoyote au hoja za kutusaidia kuyaboresha.

## Jinsi ya kutumia Mwongozo huu Wa Mwalimu

### 1. Mipango Ya Mwalimu ya Kufundishia Somo

Kurasa za kwanza katika sehemu hii zinatoa mtazamo wa somo zima kwa ufupi.

Ukurasa unaofuata utakuwa ni nakala ya ***Orodha Ya Kazi Za Darasani***. Hii orodha inaonyesha wakati ambapo kila zoezi katika Mwongozo wa Somo linatakiwa kukamilika, na wakati kila chemsha bongo na mtihani zitatolewa. Kila mwanafunzi anapaswa kupewa habari stahiki kwa ajili ya ukurasa huo mwanzoni mwa kila somo. Kitabu hiki cha Mwongozo wa Somo tayari kina nakala ambayo haijaandikwa chochote ya fomu hiyo, kwenye jalada la nyuma upande wa ndani.

Kitakachofuata ni mipango kwa ajili ya kufundishia kila somo. Hiyo yote ina kitu kinachoitwa Kweli Kuu ya Kibiblia pamoja na Mstari Mkuu. Hivyo vitu viwili vinaweza kutolewa mwanzoni mwa kipindi cha darasa. Pia vinasaidia kufanya mjadala ulenge yanayotakiwa kwa wakati wote.

Chini ya Kweli Kuu ya Kibiblia na Mstari Mkuu, kuna maelezo machache jinsi ya kufundisha somo lenyewe. Mara nyingi, marejeo yanaelekezwa kwa Mwongozo wa Mwanafunzi au kwa Zoezi linalopatikana katika Mwongozo wa Somo.

Kila somo humalizika kwa shughuli ya kufanya katika "Kufanyia Kazi Somo Maishani." Umuhimu wa kipengele hiki hauelezeki. Wakristo wapya wanahitaji mwongozo ulio wazi kuhusu jinsi ya kuanza kufanyia kazi mafundisho haya katika maisha yao ya kila siku. Hakikisha kwamba unatoa nafasi ya kutosha ya kuwasaidia wanafunzi wako kuanzisha shughuli hii.

Mwisho wa kila mpango wa kufundishia somo, kuna orodha ya kazi za wanafunzi kufanya.

Mengi katika masomo haya yalikusudiwa kuwa na vipindi vitano vya darasa, kila kimoja kikidumu kwa saa moja. Kipindi cha mwisho darasani ni kwa ajili ya mtihani. Masomo yote 14 katika mfululizo huu yanaweza kukamilishwa katika kipindi cha miezi kati ya mitatu hadi

minne, kama darasa litakutana kwa siku tano kwa wiki. Ikiwa darasa ni la saa moja tu kwa juma, unaweza kukamilisha somo moja kwa mwezi – na mfululizo wote kwa mwaka mmoja hivi. Mengi ya masomo haya yanaweza kupanuliwa na kufundishwa kwa muda mrefu, au kwa madarasa zaidi.

## 2. Mwongozo Wa Mwanafunzi

Kitabu hiki cha Mwongozo wa Mwanafunzi kinaweza kutimiza makusudi mawili. Unaweza kutaka wanafunzi wasome kurasa husika ili kujiandaa kwa ajili ya somo linalofuata. Au, unaweza kuwataka wakisome baada ya wewe kufundisha somo, ili iwe kama marudio na kama njia ya kusisitiza na kukazia kilichofundishwa darasani.

Tunakutia moyo uwaambie wanafunzi wajiandikie kumbukumbu darasani, hata ingawa utawapa Mwongozo Wa Mwanafunzi. Wanayojiandikia wenyewe pamoja na mazungumzo na mijadala darasani yatawasaidia sana kuelewa vizuri baadhi ya mada zinazoshughulikiwa katika Mwongozo Wa Mwanafunzi.

## 3. Mwongozo Wa Somo

Mazoezi yaliyo katika Mwongozo wa Somo yameandaliwa ili kumpa mwanafunzi kazi ya kufanya nje ya darasa. Baadhi ya kazi-mradi hizo zinasaidia kumwandaa mwanafunzi kwa ajili ya somo la darasa linalofuata.

Mengi ya mazoezi haya yamekusudiwa kuwasaidia wanafunzi wajikite ndani zaidi na kutazama baadhi ya maswala yanayojadiliwa darasani kwa kina. Lengo kuu la kazi hizo nyingi ni kuwaasaidia wanafunzi wagundue njia za kufanyia kazi hizo za kweli za Biblia katika maisha yao ya kila siku.

## 4. Mtihani Wa Mwanafunzi na Funguo la Majibu ya Mtihani

Mitihani hii imeandaliwa ili kutoa kipimo rahisi tu cha maendeleo ambayo kila mwanafunzi alipata katika uelewa wa kweli za Biblia zinazoshughulikiwa katika somo hili. Karatasi ya Majibu kwa ajili ya mtihani husika iko mara tu baada ya ukurasa wa mwisho wa ile nakala mfano ya mtihani wa mwanafunzi, katika Mwongozo huu wa Mwalimu.

## 5. Cheti Cha Somo

Cheti cha somo ni kwa ajili ya kuwatambua wale wanaomaliza kazi yote inayotakiwa kwa ajili ya somo hili na kufaulu mtihani. Mfano wa cheti hicho cha somo upo katika ukurasa wa mwisho wa kitabu hiki cha Mwongozo wa Mwalimu. Cheti cha Kufuzu pia kinapatikana kwa wale wanafunzi wanaomaliza masomo yote 14 katika mfululizo huu wa *Mafunzo ya Vikundi Ya Maisha Mapya*. Pia, mfano upo katika kile kitabu kinachoitwa ***Kuwatambulisha waalimu kwa Mafunzo ya Vikundi Yanayohusu Maisha Mapya***.

# Jinsi Masomo Haya Yalivyotokea

Sulemani alisema, hakuna kitu kipya chini ya jua. Maneno hayo yanaweza kufaa hata kuhusu masomo haya. Mawazo yake mengi si mapya. Tunataka kutoa shukrani zetu maalum kwa Taasisi Ya Kanuni Za Maisha (Institute in Life Principles) kwa ushawishi mkubwa katika maisha ya watu waliotayarisha masomo haya. Masomo mengi yana alama za huduma hiyo ya Taasisi Ya Kanuni Za Maisha (Institue in Life Principles).

Nataka pia kutoa shukrani zangu za dhati kwa walimu wengi sana na maelfu ya Wakristo wapya ambao wametumia masomo haya katika kipindi cha miaka kadhaa iliyopita. Mawazo yao yamekuwa na mchango mkubwa sana katika maandalizi ya masomo haya.
Pia ninamshukuru sana Ndugu Don Wilkerson kwa kunipa nafasi ya kufanya kazi katika kituo cha huduma ya Teen Challenge pale Brooklyn, New York, tokea mwaka wa 1971 hadi 1975. Katika miaka hiyo ndipo matayarisho yalipoanza ya masomo haya yaitwayo *Mafunzo ya Vikundi Yanayohusu Maisha Mapya*.

Toleo la tano la *Mafunzo ya Vikundi Yanayohusu Maisha Mapya* lilitayarishwa kwa msaada wa kamati ya Mitaala ya huduma ya Teen Challenge Marekani. Natoa shukrani maalum kwa wote waliosaidia katika mapitio na marekebisho hayo.

# Sera Kuhusu Kunakili Machapisho Haya

Vitabu vya Mwalimu na kila kitu cha mwanafunzi kinachohusiana na masomo haya ya *Mafunzo ya Vikundi Yanayohusu Maisha Mapya* kinalindwa na Sheria za Haki Miliki. Mpango maalum umefanywa ili kufasiri masomo haya kwa lugha hii ya Kiswahili. Masomo haya yanaweza kuchapwa na kupatianwa kwa ajili ya matumizi katika huduma za Teen Challenge na zinazofanana nazo, katika makanisa ya mahali fulani, shule na mashirika mengine na hata watu binafsi. Pia, yanaweza kupatikana kwenye mtandao kwa tovuti hii: www.iTeenChallenge.org Lakini, yasiuzwe. Yatolewe bila malipo. Kwa wanaotaka kuchapisha na kuuza, wapate ruhusa kwa maandishi kutoka kwa Global Teen Challenge.

Dave Batty

# Pendekezo Kuhusu Mpangilio Wa Kufundisha

Somo hili ni moja kati ya 14 katika mfululizo wa *Mafunzo ya Vikundi Yanayohusu Maisha Mapya*. Masomo yote 14 yameorodheshwa hapa kama pendekezo la jinsi ya kuyafundisha. Mfuatano huu ulitayarishwa kwa ajili ya ufundishaji endelevu wa masomo haya. Tunaweza kuutazama kama picha ya gudurumu lenye vyuma kumi na vinne. Masomo haya hayategemei linalotangulia. Kila somo linasimama lenyewe. Basi, mwanafunzi anaweza kujiunga na madarasa wakati wowote na akaingia tu vizuri kwenye mfumo.

1. Nawezaje Kujua Mimi Ni Mkristo?
2. Kuitazama Biblia Kwa Haraka
3. Mtazamo
4. Majaribu
5. Maisha Ya Kikristo Yenye Mafanikio (ni pamoja na mafunzo juu ya huduma ya Roho Mtakatifu.)
6. Kukua kupitia kufeli
7. Kanuni za Kikristo (Mahusiano Katika Kanisa La Mahali)
8. Utiifu kwa Mungu
9. Utiifu kwa Mwanadamu
10. Hasira na Haki za Kibinafsi
11. Jinsi Ya Kujifunza Biblia
12. Kujipenda na Kujikubali Mwenyewe
13. Mahusiano yako wewe Binafsi na Wengine
14. Nguvu Ya Kiroho na Mambo Yasio Ya Kawaida

Tazama kitabu kiitwacho, ***Kuwatanguliza waalimu kwa Mafunzo ya Vikundi Yanayohusu Maisha Mapya***, ili kupata maelezo zaidi juu ya kufundisha masomo hayo.

# Mipangilio ya Masomo

# Kwa Mwalimu

Angalia ukurasa wa 4 wa Mwongozo wa Mwalimu kwa habari zaidi
kuhusu matumizi ya mipangilio hii ya masomo.

# Maelezo ya kozi kwa jumla

1. Unaweza kutanguliza kozi hii kwa wanafunzi siku moja au mbili kabla ya kipindi cha kwanza darasani na kuwapa kazi zao za kwanza. Ikiwa inawezekana wape wanafunzi Mwongozo wa Somo siki moja au mbili kabla ya kuanza kufundisha kozi hii. Mwongozo wa Mwanafunzi unaweza kutolewa kwa wanafuzi wakati wowote. Wape kazi ya kusoma Sura ya 1, ambayo itajadiliwa katika kipindi cha kwanza darasani.

2. Kwenye ukurasa unaofuata kuna *Orodha ya kazi za Darasani* unaotoa tarehe ambayo kila kazi inapaswa kukamilishwa. Waagize wanafunzi wako kujaza tarehe zinazofaa katika nakala tupu kwenye *Orodha ya kazi za Darasani* iliyo nyuma ya Mwongozo wao wa somo.

3. Watarifu wanafunzi kuwa wanapaswa kukamilisha Zoezi la 1 kwenye Mwongozo wa Somo wanapohudhuria kikao cha kwanza cha darasa.

4. Kila mpango wa somo unatoa shughuli moja au zaidi ya kutambulisha somo. Kusudi kuu la kufanya haya ni kuwasaidia wanafunzi kuwa makini katika mada kuu ya somo hilo. Tunataka kuunda mazingira mazuri na yenye uwazi yatakayowafanya wanafunzi wote kuhisi huru kushiriki katika majadiliano darasani.

   Kumbuka, Kichangamshi cha somo la 3 kuhusu suala la kuwa meneja wa Mungu, kinakuhitaji mahojiano na mtu ambaye amewahi au anafanya kazi kama msimamizi wa biashara. Chagua ni nani utakayemhoji mapema kutoka kwa darasa lako, au umtafute mtu atakayejitolea kutoka kwa kanisa lako au marafiki ambao wako tayari kuja kwenye darasa lako kwa mahojiano hayo.

5. Unapaswa kuamua ni vipindi vingapi vya darasa unayotaka kutumia kufundisha kozi hii. Kuna mipangilio ya masomo kwa vipindi 7 vya darasa kwenye kurasa zifuatazo. Kama ni lazima upunguze viwe vipindi 4 vya darasa na cha 5 kiwe cha mtihani, basi unapaswa kuamua ni mada gani utakayounganisha kuwa kipindi kimoja cha darasa.

# Orodha ya Kazi za Darasani

**Jina la Kozi** Kanuni za Kikristo

**Chemsha Bongo** Mistari ya Kukariri Tarehe

| | Mistari ya Kukariri | Tarehe |
|---|---|---|
| 1 | Waefeso 4:29 | Somo La 2 |
| 2 | 2 Wakorintho 9: 7 | Somo La 3 |
| 3 | Wakolosai 3:23 | Somo La 4 |

**Zoezi** Jina La Kazi Tarehe ya Kuwasilisha

| | Jina La Kazi | Tarehe ya Kuwasilisha |
|---|---|---|
| 1 | Ufafanuzi | Siku Ya 1 |
| 2 | Ushuhuda Wangu | Siku Ya 3 |
| 3 | Meneja wa Mungu | Siku Ya 3 |
| 4 | 2 Wakorintho 9:7 | Siku Ya 4 |
| 5 | Kazi Yangu | Siku Ya 4 |
| 6 | Ubatizo wa Maji | Siku Ya 5 |

**Mtihani** Tarehe Siku Ya 7

1

# Somo la 1
# Kanisa La Mahali Pamoja

**1. Kweli kuu ya Kibiblia**

Ninaweza kufurahia kanisa kwa kuhusika kwa kuzungumza na na watu kanisani.

**2. Mstari mkuu: Waefeso 4:16 (Biblia Takatifu (SUV))**

Katika yeye mwili wote ukiungamanishwa na kushikanishwa kwa msaada wa kila kiungo, kwa kadiri ya utendaji wa kila sehemu moja moja, huukuza mwili upate kujijenga wenyewe katika upendo.

**3. Mafundisho ya mwanafunzi yaliyotumiwa katika somo hili**

Sura ya 1 kwenye Mwongozo wa Mwanafunzi inaenda pamoja na somo hili.
Zoezi la 1 kwenye Mwongozo wa somo “Ufafanuzi” litatumika katika somo hili.

**4. Zoezi la utangulizi wa somo (Dakika 5)**

Wape wanafunzi 2 au 3 fursa ya kuzungumzia kumbukumbu yao ya kwanza walipoingia kanisani. Baadhi ya wanafunzi wako wanaweza kuwa wamelelewa katika familia ambazo zilienda kanisani mara kwa mara. Ikiwa hayo ndiyo majibu unapata kutoka kwa swali hili, unaweza kuliuliza kwa njia nyingine ili kuona kama unapata jibu tofauti.

Ni wangapi kati yenu walikuwa Wakristo wakiwa vijana au watu wazima?
Ni kumbukumbu gani ulizo nazo za kanisa kabla ya kuwa Mkristo?

Hatutafuti majibu yoyote sahihi au yasiyosahihi hapa. Taja kuwa maisha yetu ya zamani ya kwenda kanisani yanaweza kuwa na athari kubwa kwa mitazamo yetu ya sasa kwa makanisa.

**5. Jadili Hoja A. “Je, Neno “kanisa” linamaanisha nini?”**
**(Dakika 5-10 Mwongozo wa Mwanafunzi ukurasa wa 4-5)**

Kwa kutumia Zoezi1 la Mwongozo wa Somo, swali 1, waambie wanafunzi wafafanuwe neno “kanisa.” Baada ya kutoa maelezo yao, jadili kwa kifupi maelezo tofauti ya neno “kanisa” kwenye ukurasa 4-5 katika Mwongozo wa Mwanafunzi.

Wakati unawasilisha hoja zilizo chini ya hoja ndogo ya 3, “Taaswira za kanisa katika Biblia,” fanya mawasilisho yawe mafupi. Hakikisha wanaelewa tu kuwa wakati wanasoma maandiko ambayo yanataja picha hizi, lazima watafsiri maana kama picha au ishara.

**6. Jadili Hoja B. “Kwa nini tuna kanisa la mahali pamoja?”**
**(Dakika 10-15 Mwongozo wa Mwanafunzi ukurasa wa 5)**

Unapo wasilisha hoja hizi mbili, unaweza kupata kwamba watu wengine, ikiwa ni pamoja na wale ambao wamekuwa wakienda kanisani kwa miaka mingi, wanaweza kutokubaliana na vipaumbele vya hoja hizi mbili.

Unapowasilisha hoja hizi mbili, sisitiza kuwa zote ni muhimu. Ikiwa kanisa litapuuza moja wapo ya madhumuni haya, litakosa mengi ambayo Mungu anataka lipate.

Kwa kifupi wasilisha sababu mbili kuu za kuwa na kanisa la mahali pamoja.
Zidi kurejelea sababu hizi katika kozi hii yote.

Hakikisha umesisitiza umuhimu wa kila mtu, haswa Wakristo wapya wa kushiriki katika kanisa la mahali pamoja. Haya sio maoni - ni muhimu kwa ukuaji wao wa kiroho.

Kuna makanisa ambayo huwafanya watu kufikiria kwamba wanapojiunga na kanisa hivyo basi wameokolewa. Jadili swala hili kwa makini na uhakikishe kuwa wanafunzi wako wanaelewa kuwa kwenda kanisani hakumfanyi mtu kuwa Mkristo.

Ikiwa unafundisha kozi hii katika kikao cha Changamoto kwa Vijana, sisitiza kwa wanafunzi umuhimu mkubwa wa kuwa sehemu ya kanisa la mahali pamoja wanapomaliza kozi

## B. Kwa nini tuna kanisa la mahali pamoja?

1. Kusaidia Wakristo kukua kwa nguvu kiroho.

2. Kuwaambia kuhusu Kristo wale ambao si Wakristo.

*Imenukuliwa kutoka kwa Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 5*

**7. Tambulisha Hoja C, Ninawezaje kufurahishwa na kanisa?**
**(Dakika 3-5 Mwongozo wa Mwanafunzi ukurasa wa 5-6)**

Mara nyingi Wakristo wapya huhisi kama wageni wanapotembelea kanisa lilo karibu nao. Unapotanguliza sehemu hii, eleza umuhimu wa kwenda kanisani.
Katika jamii nyingi, kuna makanisa mengi ambayo unaweza kuchagua unapofanya uamuzi wa ni wapi utahudhuria. Tunapaswa kusisitiza umuhimu wa kuchagua kanisa ambalo litawapa chakula kizuri cha kiroho na ushirika na Wakristo waliokomaa.

Eleza kuwa katika sehemu hii ya kipindi cha darasa tutachunguza viungo 4 muhimu vya kutafuta kanisa ambalo litakuwa na athari nzuri katika maisha yao.
Unaweza kuorodhesha maswala manne tutakayojadili, kisha ujadili kila moja kwa undani, kama ilivyoelezwa katika hoja 4 zifuatazo za mpangilio huu wa somo.

Hoja hizi 4 zinaweza kutumika kama njia ya kuchagua kanisa lenye afya.

## C. Ninawezaje kufurahishwa na kanisa? (Matendo 2:42)

1. Tunakusanyika pamoja kwa ushirika.
2. Tunakusanyika pamoja kumwabudu Mungu na kuomba.
3. Tunakusanyika pamoja kumsikiliza Mungu.
4. Tunakusanyika pamoja ili kusaidiana.

*Imenukuliwa kutoka kwa Mwongozo wa Manafunzi, ukurasa wa 5-8*

Unaweza kuunda bango lililo na orodha ya hoja hizi 4 na uliweke ukutani unapoanza mjadala huu.

**8. Jadili Hoja C-1, "Tunakusanyika pamoja kwa ushirika."**
**(Dakika 5-7 Mwongozo wa Mwanafunzi ukurasa wa 5-6)**

Sababu ya kwanza ya kuhudhuria kanisa lilo karibu ni kwa kuwa na ushirika na Wakristo wengine. Mungu hakutuita tuwe Wakristo "Wapweke" – Anataka tuwe na uhusiano na wengine.

Mwongozo wa Mwanafunzi umeorodhesha njia 5 tunazoweza kutumia kuishi katika ushirika na Wakristo wengine. Chukua muda wa kujadili kila moja ya hizi, ukitumia mifano ya kibinafsi kutoka kwa wanafunzi wako darasani.

## Jinsi kuwa na ushirika na Wakristo wengine kunatusaidia

a. Unatusaidia kujua Wakristo wengine
b. Hutupatia fursa ya kujadili imani zetu
c. Unatuonyesha jinsi ya kujifunza kupenda wengine
d. Unatusaidia kufahamu njia za kusaidiana
e. Hutusaida kuombeana

*Mwongozo wa Mwanafunzi ukurasa wa 5-6*

Wakati mwingine Wakristo wapya huwa na wakati mgumu wa kuwafikia watu wapya ili kukuza urafiki. Sisitiza umuhimu wa kuchukua hatua ya kuanzisha urafiki mpya. Hawawezi kusubiri wengine wawafikie.

Marafiki wacha Mungu wanaweza kuwa sehemu muhimu katika ukuaji wao wa kiroho.

**9. Jadili Hoja C-2, "Tunakusanyika pamoja kumuabudu Mungu na kuomba." (Dakika 5-7 Mwongozo wa Mwanafunzi ukurasa wa 6)**

Sababu ya pili ya kuhudhuria kanisa mahalia ni kwa kusudi la kumwabudu Mungu na kuomba na Wakristo wengine.

Tunapaswa kujifunza jinsi ya kumwabudu Mungu. Mwongozo wa Mwanafunzi unafafanua neno "kuabudu," – kumwambia mtu ni wa thamani kwako; kusifu; kupendezwa; kuheshimu; kustahi.

Tunapaswa kujifunza jinsi ya kutenda haya maishani mwetu kwenye uhusiano na Mungu. Njia mbili za kawaida za kufanya hivi ni kupitia kwa nyimbo tunazoimba ambazo zinaelekezwa kwa Mungu, na kwa maombi yetu.

Sisitiza umuhimu wa kufanya hivi na wala sio tu mara moja kwa wiki kanisani, mbali kufanya mambo haya mawili kuwa sehemu ya kawaida ya ratiba yetu ya kila siku.

Biblia imejaa mifano mingi ya watu waliomwabudu Mungu. Zaburi nyingi zinaonyesha namna za kuabudu. Wahimize wanafunzi wako kusoma Biblia ili kuona jinsi watu walivyomwabudu Mungu. Wahimize wasome sala hizi za ibada na wazibinafsishe. Wafanye yawe maombi yao ya ibada.

Jambo lingine muhimu la kusisitiza hapa ni kwamba, ibada haipaswi kuwa ya kibinafsi tu. Wanapaswa kuvunja ganda lao la kibinafsi, na kujifunza jinsi ya kumwabudu Mungu pamoja na wengine. Sisi ni sehemu ya familia moja maalum ya Mungu na anachotaka Mungu kutoka kwetu ni tumuabudu kwa pamoja.

Unaweza kuwaambia wanafunzi kuwa tutatumia kipindi cha darasa zima kushughulikia mada ya maombi baadaye katika kozi hii na utumie muda mfupi tu kwa somo hili la maombi.

**10. Jadili Hoja C-3, "Tunakusanyika pamoja kumsikiliza Mungu." (Dakika 5-7 Mwongozo wa Mwanafunzi ukurasa wa 6-7)**

Sababu ya tatu ya kuhudhuria kanisa lilo karibu nawe ni kwa sababu ya kumsikiliza Mungu.

Mwongozo wa Mwanafunzi unataja njia 5 tofauti za kusikia kutoka kwa Mungu. Ikiwa unataka kuongeza njia zingine, pia ni sawa, lakini kumbuka lengo letu hapa ni kuonyesha jinsi kanisa linaweza kusikia kutoka kwa Mungu.

## Jinsi Mungu huongea nasi

a. Kupitia kwa Biblia
b. Kupitia kwa maombi
c. Kupitia kwa karama za Roho Mtakatifu
d. Kupitia kwa Wakristo wengine wacha Mungu
e. Kupitia kwa hali mbalimbali za maisha

*Imenukuliwa kutoka kwa Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 6-7*

Sisitiza mambo mawili ya msingi hapa:

1. Mungu anataka kuwasiliana na kila mmoja wetu.
   Anatupenda sana, na anatamani mawasiliano ya kibinafsi.

2. Tunapaswa kuwa na mtazamo wa kutarajia kusikia kutoka kwa Mungu, na kutaka kusikia kutoka kwa Mungu.

Suala la kusikia kutoka kwa Mungu linahitaji kuwekwa katika kiwango cha matendo. Kuwasiliana na watu wanaoishi karibu nawe ni sehemu ya kawaida ya kila siku. Vivyo hivyo, tunapaswa kuona kuwa kusikia kutoka kwa Mungu ni sehemu ya kawaida ya siku zetu.

Hii haimaanishi kwamba tutamsikia Mungu akinena kwa sauti ambayo tunaweza kusikia kwa masikio yetu - ingawa wakati mwingine watu husikia kutoka kwa Mungu kwa njia hiyo.

Tutasikiaje kutoka kwa Mungu? Orodha iliyotolewa katika Mwongozo wa Mwanafunzi kwenye ukurasa wa 6 inaanza kwa njia ya kawaida tunayoweza kusikia kutoka kwa Mungu-kusoma Biblia.

Tunapohudhuria kila ibada ya kanisa, tunapaswa kuwa na mtazamo wa “Mungu, nataka kusikia kutoka kwako leo.” Katika kila sehemu ya huduma tunapaswa kusikiliza kwa moyo wetu kile ambacho Mungu anataka kusema nasi.

Mungu anaweza kuweka mawazo moyoni mwako ambayo yanazungumza moja kwa moja na shida unayokabiliana nayo. Au pengine unakabiliwa na uamuzi mkubwa, na unahitaji hekima ya Mungu katika kufanya uamuzi huo. Kuwa na matarajio kuwa Mungu atazungumza nawe kupitia sehemu mbali mbali za huduma ya kanisa.

Taja kuwa njia nyingine ya kawaida ambayo Mungu huzungumza nasi ni kupitia kwa ujumbe uliohubiriwa na mchungaji. Eleza maswala haya 2 kwa makini.

1. Mungu anaweza kuzungumza nawe kupitia yale mchungaji anasema. Wakati mwingine watu husema, “Yale mchungaji alisema yalizungumza nami moja kwa moja na kunisaidia katika suala ambalo nilikuwa nikipambana nalo.” Huyo ni Mungu anayefanya kazi — anasema nawe!

2. Si kila kitu mchungaji anasema ni neno la moja kwa moja kutoka kwa Bwana. Itakuwa vyema kutaja kuwa kile mchungaji anasema katika mahubiri yake kinaweza kuwa:

   a. Neno la Mungu - haswa wakati anasoma kutoka kwenye Biblia

   b. Maelezo ya neno la Mungu-na kufanya hivi kwa njia iliyo sawa na sahihi

   c. Maoni ya mchungaji. Maoni haya yanaweza kujazwa na hekima ya kiungu, au kinyume - maoni haya yanaweza kuwa mbali na msimamo wa Mungu juu ya suala hilo.

Lazima tuwe makini kujifunza jinsi ya kutathmini kile tunachosikia kanisani na kutenganisha ukweli wa Mungu na maoni ya mwanadamu. Ni sawa ikiwa haukubaliani na maoni ya mtu mwingine, lakini lazima tuwe makini kufahamu na kutii ukweli wa Mungu.

Tunapowasilisha yaliyomo kwenye kipindi hiki, tunapaswa kuwa waangalifu ili tusije tukageuza haya kuwa majadiliano ya jinsi Mungu anavyonena nasi katika kila sehamu ya maisha yetu — hilo ni suala pana mno la kushughulikiwa katika sehemu hii ya somo. Tunataka kuangazia jinsi tunaweza kusikia kutoka kwa Mungu katika muktadha wa kanisa.

Itakuwa vyema kusema kuwa kanisa ni zaidi ya huduma halisi ya kanisa. Mungu anaweza kusema nasi kupitia huduma zingine za kanisa ambazo si za Jumapili asubuhi.

Malizia hatua hii kwa kusisitiza umuhimu wa usawa hapa. Tunapaswa kutarajia kusikia kutoka kwa Mungu, lakini pia tunapaswa kuwa waangalifu ili tusiwategemee sana watu wengine kutupatia neno kutoka kwa Bwana. Tunapaswa kujifunza jinsi ya kujaribu kila "maneno kutoka kwa Bwana" kwa kusoma Biblia kwa makini. Haijalishi ikiwa ushauri wa mtu unaonekana kuwa wa kiroho, tunapaswa kuona ikiwa unakubaliana na yale ambayo Biblia inasema.

Ikiwa mtu  anakukaribia na kukwambia, "Nina neno kutoka kwa Bwana kwamba utafunga ndoa na mtu huyu," utajuaje ikiwa kweli amekuletea neno kutoka kwa Mungu? Ikiwa tayari umeolewa na mtu mwingine, basi utafahamu mara moja kwamba si kutoka kwa Mungu. Huna haja ya kuomba na kumwuliza Mungu ikiwa unapaswa kutalikiana na mumo na kumuoa mtu huyu anayezungumziwa na mtu aliyekuletea "neno kutoka kwa Bwana."

Usawa ndio ufunguo wa uhusiano wa karibu na Mungu.

**11. Jadili Hoja C-4, "Tunakusanyika pamoja ili kusaidiana."**
**(Dakika 5-7   Mwongozo wa Mwanafunzi ukurasa wa 7-8)**

Sababu ya nne ya kuhudhuria kanisa lilo karibu nawe ni kutumia fursa hii kuweza kuwasaidia wengine na pia kupokea msaada. Hatuji tu kanisani kushiriki katika huduma ya kanisa na kisha kurudi nyumbani. Mungu anataka kanisa liwe pahali pa watu kupata msaada.

Mara nyingi Wakristo wapya huhisi kama wageni kanisani. Hawahisi kama wameshikamana na watu wengine huko. Njia moja ya kuanza kutatua tatizo hilo ni kutafuta fursa za kuwasaidia watu wengine.

Mahali pa kuanzia ni kwa kumuuliza mchungaji, "Ninaweza kufanya nini kuwasaidia wengine? Ninataka kushiriki ili kusaidia watu."

Wakati huo huo, unapaswa kumwuliza Mungu, "Mungu, unataka nihusike wapi kusaidia watu?" Hii haimaanishi lazima upokee ishara maalum kutoka kwa Mungu kabla ya kufanya lolote. Suala muhimu hapa ni kwamba tunatarajia Mungu kufungua milango ambayo anataka tuhusike nayo, na kufunga milango ambayo hataki tuhusike.

Sisitiza kwa wanafunzi wako kwamba, kuwa sehemu ya kanisa lililo karibu nawe inamaanisha kwamba tunahusika katika kuwasaidia wengine. Hauchagui-ni sharti. Si kwa nyota ya wachache tu — Mungu ana jambo la kufanywa na na kila mmoja wetu.

Tusifuate tu tamaa zetu za ubinafsi, tuwatafute wengine walio na mahitaji na kumwuliza Mungu jinsi tunavyoweza kuwa sehemu ya mchakato Wake wa kuwasaidia.

**12. Matumizi binafsi (dakika 5-10)**

Wahimize wanafunzi wako kuzingatia matumizi ya kibinafsi ya kuomba moja kwa moja kwa kanisa lao. Waambie waangalie tena sababu 4 kuu katika Hoja C. "Ninawezaje kufurahishwa na kanisa?" Waambie wapime kiwango kwa kutumia haya — ni zipi wanahitaji kutumia kwa njia kubwa maishani mwao? Waagize waandike lengo maalum la yale wataanza kufanya wiki itakayofuata.

Ikiwa hii inafundishwa katika mpangilio wa makazi kama vile Changamoto kwa Vijana, angazia matumizi ya kibinafsi kwenye maswala haya matatu.

A. Sisitiza umuhimu wa kuweka lengo la kuchagua kanisa la kuhudhuria watakapohitimu kutoka kwa mpangilio huo.

B. Wahimize kutumia alama hizi 4 muhimu kwa kanisa wanalohudhuria kwa sasa wakiwa bado kwa mpangilio huu. Wanaweza kukosa kutumia kikamilifu hoja hizi nne, lakini wahimize wafanye kadri wawezavyo sasa hivi.

C. Pia wahimize watumie vidokezo hivi 4 muhimu kwa uhusiano wao na wale ambao wanaishi nao katika programu kwa sasa. Wasaidie kuona kwamba kanisa sio tu la mikutano ya Jumapili, bali ni la kuwa na uhusiano na Wakristo wengine.

**13. Kazi**

A. Ikiwa haujafanya hivyo, wape Mwongozo wa Mwanafunzi leo.
Waambie wanafunzi wasome Sura ya 2 "Jinsi ya kutoa ushuhuda," katika maandalizi ya kipindi cha daraasa kijacho.

B. Sahihisha Mwongozo wa Somo, Zoezi la 1, "Ufafanuzi."

C. Zoezi la 4 la Mwongozo wa Somo, "2 Wakorintho 9: 7," halitasahihishwa hadi kipindi cha 4 cha darasa. Hata hivyo, unaweza kuwahimiza wanafunzi wako kuanza zoezi hili mara moja, kwa sababu linaweza kuwasaidia wanapofanya zoezi la 2 la kuandika ushuhuda wao wa kibinafsi. Eleza kuwa lengo la zoezi la 4 ni kuwapa wanafunzi maoni ya jinsi ya kukumbuka Maandiko maalum ambayo wametumia katika maisha yao ya kibinafsi ya kila siku.

**14. Tathmini ya Somo**

Tafadhali orodhesha maoni yako kuhusu oboreshaji wa somo hili.
Ni sehemu zipi zilifanya kazi bora zaidi?
Ni sehemu zipi zilikuwa gumu zaidi kwa wanafunzi kuelewa?
Ni nini kilionekena kuwa cha msaada zaidi kwa wanafunzi wako?

# Somo la 2
# Jinsi ya kutoa ushuhuda

2

**1. Kweli kuu ya Kibiblia**

Wakati ninatoa ushuhuda, ninaweza kuwaambia wengine jinsi Mungu ananisaidia kukua.

**2. Mstari mkuu: Waefeso 4:29 (Biblia Takatifu (SUV))**

Neno lo lote lililo ovu lisitoke vinywani mwenu, bali lililo jema la kumfaa mwenye kuhitaji, ili liwape neema wanaosikia.

**3. Mafundisho ya mwanafunzi yaliyotumiwa katika somo hili**

Sura ya 2 kwenye Mwongozo wa Mwanafunzi inaenda pamoja na somo hili. Zoezi la 1 kwenye Mwongozo wa somo litatumika katika somo hili.

**4. Zoezi la utangulizi wa somo (dakika 5-7)**

Anza kipindi cha leo cha darasa kwa kuuliza mtu mmoja au wawili wajitolee kusema jinsi ushuhuda wa mtu mwingine uliathari maisha yao kibinafsi. Unaweza kupanga haya mapema kabla kuanza kwa kipindi cha darasa ili ujue ni nani atazungumza katika shughuli hii ya darasa.

Ikiwa mtu alikuwa Mkristo mara ya kwanza akiwa kijana au mtu mzima, wanaweza kukumbuka athari ya ushuhuda wa mtu mwingine katika kuwashawishi kuhusu umuhimu kuwa Mkristo.

**5. Jadili Hoja A, “Ushuhuda ni nini?”**
**(Dakika 5 Mwongozo wa Mwanafunzi ukurasa wa 9)**

Kabla ya kujadili yaliyo katika Mwongozo wa Mwanafunzi, waulize wanafunzi wako kutoa ufafanuzi wao wa neno “ushuhuda.” Wahimize kurejelea maoni waliyoyaandika katika Mwongozo wa Somo zoezi la 1.

Baada ya wanafunzi wako kutoa maoni yao, waelekeze kwenye ukurasa wa 9 katika Mwongozo wa Mwanafunzi ili kujadili kwa kifupi ufafanuzi wa ushuhuda ambao tutatumia katika somo hili. Unaweza kuandika ufafanuzi huu kwenye karatasi kubwa na kuliangika darasani:

> **Ushuhuda** — kuwaeleza wengine kile Kristo amefanya na bado anafanya katika maisha yako.
>
> *Imenukuliwa kutoka kwa Mwongozo wa Mwanafunzi ukurasa wa 9*

**6. Jadili Hoja B, " Kwa nini nitoe ushuhuda?"**
**(Dakika 5-10 Mwongozo wa Mwanafunzi ukurasa wa 9)**

Kwa kifupi pitia hoja 6 zilizoorodheshwa katika Mwongozo wa Mwanafunzi ukielezea ni kwanini wanapaswa kuwa tayari kutoa ushuhuda wao.

## B. Kwa nini nitoe ushuhuda?

1. Ni njia ya kumtii Kristo. (Mathayo 28:19-20).
2. Kunanipa nafasi ya kuimarisha imani na tumaini langu kwa Mungu. Kunanisaidia kuwa Mkristo aliyeimarika zaidi.
3. Kunanipa nafasi ya kuchukua msimamo ulio wazi kwa Mungu (Matendo 5:29)
4. Kunanipa nafasi ya kuwasaidia wengine. Kunaweza kusaidia wengine kumhusisha Mungu na maisha yao.
5. Kunanipa nafasi ya kuleta utukufu kwa Mungu, kwa hivyo Yeye hupata sifa kwa mabadiliko yanayoonekana maishani mwangu.
6. Kunanipa fursa ya kumshinda Shetani. (Ufunuo 12:11)

*Imenukuliwa kutoka kwa Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 9*

Baada ya kupita hoja hizi, unaweza kuchukua dakika chache kujadili baadhi ya nafasi walizonazo za kutoa ushuhuda. Waambie wakusaidie kuunda orodha. Yafuatayo ni maoni kadhaa yaliyotolewa na waalimu na wanafunzi wa zamani – Hata hivyo wape nafasi wanafunzi wako watoe maoni yao kabla ya wewe kuongeza maoni yoyote kutoka kwa orodha ifuatayo.

Unaweza kutoa Ushuhuda wako wapi?

1. Kwa kanisa lako
2. Kwa familia yako. (Ikiwa hauishi nao, fanya hivi wakati unapowatembele, piga simu, au kuwaandikia barua.)
3. Kwa watu wanaoishi karibu nawe (haswa mpya)
4. Kwa wenzako
5. Katika mikutano ya kikundi
6. Wakati wa kula
7. Wakati wako wa kupumzika

**7. Jadili Hoja C, "Hoja kuu za ushuhuda mzuri"
(dakika 15-20 Mwongozo wa Mwanafunzi ukurasa wa 9-10)**

Fafanua tofauti kati ya ***ushuhuda*** na ***ushuhuda*** wa ***maisha*** mwanzoni mwa majadiliano yako juu ya hatua hii. Tutajadili ***ushuhuda wa maisha*** baadaye katika kipindi cha darasa. Wajulishe kwamba wanapaswa kutafuta fursa nyingi za kutoa ushuhuda wakati wa shughuli zao za kila wiki.

Haswa kwa Wakristo wapya, wengi wao wanahitaji kupata maswala mapya ya kuzungumzia badala ya kuzungumza tu juu ya maisha yao ya zamani ya dhambi. Kutafuta nafasi za kuzungumza juu ya kile Mungu anafanya katika maisha yao wiki hii ni sehemu muhimu katika ukuaji wao wa kiroho.

Wasilisha sehemu 4 za ushuhuda mzuri zilizoorodheshwa kwenye ukurasa wa 10 wa Mwongozo wa Mwanafunzi. Unapaswa kuwa tayari kutoa mifano 2 au 3 maalum inayoonyesha muundo huu wa kutoa ushuhuda. Hizi zinapaswa kuwa shuhuda ambazo wanafunzi wako wanaweza kuelewa kwa urahisi, kulingana na umri wao na ukomavu wa kiroho.

## Sehemu 4 Muhimu za Ushuhuda Mzuri

1. Eleza eneo moja katika maisha yako ya kila siku pale ambapo Mungu anakusaidia kukua.

2. Taja mstari mmoja katika Biblia ambao umekusaidia kukua katika eneo hili la maisha yako. Ikiwa umekariri aya hiyo, basi inukuu. Au soma kutoka kwa Biblia yako.

3. Eleza jinsi umeutumia mstari huu kukusaidia katika eneo hili moja la maisha yako. Usihubiri. Eleza kwa njia rahisi na inayofaa jinsi aya hii inakusaidia. Eleza jinsi aya hii inahusiana na eneo la maisha yako ambapo Mungu anakusaidia kukua.

4. Toa mfano mmoja maalum kutoka siku chache zilizopita kuonyesha jinsi ulivyotumia aya hii. Mpe Mungu sifa kwa kukusaidia kukua.

*Imenukuliwa kutoka kwa Mwongozo wa Mwanafunzi ukurasa wa 10*

Unaweza kuunda bango kubwa lililo na hoja hizi 4 kuu ili kuliweka kwenye darasa lako kwa majadiliano ya leo.

Waeleze wanafunzi wako umuhimu wa kuhakikisha kuwa ushuhuda wao umeleta utukufu kwa Mungu, sio kujiangazia wao wenyewe. Hatufanyi hivi kuwaburudisha watu wengine. Lakini ukitolewa vizuri, unaweza kuwasaidia wengine na kuwatia-moyo. Wakati wa kutoa ushuhuda wao, sio wakati wa kuhubiri.

Sehemu muhimu zaidi ya ushuhuda wao ni kutoa mfano maalum wa jinsi Mungu anavyowasaidia kukua katika sehemu maalum ya maisha yao.

Itakuwa vyema kwa wanafunzi wako kutoa ushuhuda darasani kulingana na hoja 4 kuu zilizoorodheshwa kwenye ukurasa wa 10 wa Mwongozo wa Mwanafunzi. Wape nafasi wanafunzi wengine kutathmini jinsi walivyofuata hoja nne kuu. Tahadhari isije ikageuka kuwa fursa ya kuwakosoa wale wanaotoa ushuhuda wao.

Unaweza pia kufanya hivi baadaye katika kozi hii baada ya kumaliza Zoezi la 2 la Mwongozo wa Somo ambapo wataandika ushuhuda.

Baadhi ya wanafunzi wako wanaweza kuwa na wakati mgumu kufikiria juu ya sehemu maalum katika maisha yao ambapo Mungu amewasaidia kukua. ***Mfano wa Kujifunza wa Maisha-kwa-Maisha*** kwenye ukurasa wa 10 katika Mwongozo wa Mwanafunzi unatoa mkakati mmoja wa kufahamu maswala halisi ya maisha ya kutumika katika ushuhuda.

Chukua muda wa kujadili chati hii na utoe mifano 2 au 3 ya wengine ambao wameitumia kama njia ya kupata msaada kutoka kwa Mungu maishani mwao.

**8. Jadili Hoja D, "Msaada wa Ziada"**
**(Dakika 5-10 Mwongozo wa Mwanafunzi ukurasa wa 11)**

Kwa kifupi pitia kila mojawapo wa hoja 4 zilizoorodheshwa katika sehemu hii. Wahimize wanafunzi wako waandike shuhuda zao-zilizofungwa kwa hoja # 2.

## D. Msaada wa ziada

1. Ushuhuda wako uwe mfupi, chini ya dakika tano.
2. Panga kile utakachosema katika ushuhuda wako.
3. Hakikisha ushuhuda wako wote unaleta utukufu kwa Mungu.
4. Omba Roho Mtakatifu akusaidie kusema mambo yanayofaa.

*Imenukuliwa kutoka kwa Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 11*

Hoja 2 za mwisho haziwezi kupuuzwa ikiwa tutafanya vyema kwa kutoa ushuhuda kwa wengine. Wahimize pia kuepuka "dhambi" ya kuwa kimya. Ibilisi atajaribu kuwafanya wasiseme lolote — Uoga unaweza kuwa njia yake ya kuwafanya wawe kimya. Tunapaswa kutafuta fursa za kutoa ushuhuda wetu, na tutaona Mungu akitusaidia kushinda woga huo.

**9. Jadili Hoja E, "Kutoa ushuhuda wa maisha yako"**
**(Dakika 5-10 Mwongozo wa Mwanafunzi ukurasa wa 12)**

Onyesha kuwa ***ushuhuda wa maisha*** si historia yako yote ya maisha. Hadithi ya maisha yako ni wasifu. Waambie wanafunzi wako waandike kitabu ikiwa wanataka watu wapate hadithi yao yote ya maisha.

Kwa kifupi pitia kila moja ya hoja 4 zilizoorodheshwa katika sehemu hii. Mwongozo wa Mwanafunzi unatoa maoni ya ziada kwa sehemu hizi 4 za ushuhuda wa maisha.

Mara nyingi katika Changamoto kwa Vijana, wanafunzi wana nafasi ya kutoa ushuhuda wao wa maisha wanapotembelea makanisa. Sisitiza kwa wanafunzi wako umuhimu wa kutoa ushuhuda maalum. Hawana haja ya kuzungumzia dhambi zote walizofanya katika maisha yao ya zamani. Wanapaswa tu kutoa mfano maalum wa maisha yao ya zamani ya dhambi, na kuelezea jinsi ulileta uchungu na uharibifu katika maisha yao.

Wanapaswa kutumia angalau wakati sawa, ikiwa si zaidi kueleza jinsi walivyompokea Kristo maishani mwao, na ni mabadiliko gani yamefanyika tangu wakati huo.

Ushuhuda wao wa maisha unapaswa pia kujumuisha angalau mstari mmoja wa Biblia ambao umewasaidia kukua katika uhusiano wao wa kibinafsi na Yesu.

Wahimize wanafunzi wako kuandika ushuhuda wao wa maisha.

## E. Kutoa ushuhuda wa maisha yako

1. Eleza matokeo ya dhambi.
2. Eleza jinsi ulivyofikia hapa na jinsi ulivyokuwa Mkristo.
3. Eleza jinsi maisha yako yalivyobadilika tokea ulipokuwa Mkristo.
4. Waambie mipango na malengo ya maisha yako ya siku za zijazo.

*Imenukuliwa kutoka kwa Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 12*

**10. Matumizi Binafsi (dakika 5-10)**

Kwa matumizi ya kibinafsi leo, wahimize wanafunzi watoe ushuhuda kanisani, katika ibada ndogo za vikundi, au ana kwa ana kwa mtu mwingine. Wahimize wafanya hivi ndani ya siku chache zijazo, sio miezi kadhaa kutoka sasa.

**11. Kazi**

A. Wape maswali kutoka Waefeso 4:29 mwishoni mwa kipindi cha darasa.

B. Wape Zoezi 2 la Mwongozo wa Somo, “Ushuhuda wangu”, na Zoezi 3, “Meneja wa Mungu,” ambazo zinapaswa kukamilika kabla ya kipindi kijacho cha darasa.

C. Wape nafasi wanafunzi wako wasome Sura ya 3 kutoka kwa Mwongozo wa Mwanafunzi ili kujiandaa kwa kipindi kijacho cha darasa.

D. Kipindi chetu kijacho cha darasa kitashughulikia suala la kuwa meneja wa Mungu. Uliza ikiwa kuna mtu yeyote darasani ambaye amewahi au kwa sasa anafanya kazi kama meneja katika biashara. Waambie wazungumze nawe baada ya darasa na kisha uwaeleze jinsi utakavyowahoji mwanzoni mwa kipindi kijacho cha darasa.

## 12. Tathmini ya Somo

Tafadhali orodhesha maoni yako kuhusu oboreshaji wa somo hili.
Ni sehemu zipi zilifanya kazi bora zaidi?
Ni sehemu zipi zilikuwa gumu zaidi kwa wanafunzi kuelewa?
Ni nini kilionekena kuwa cha msaada zaidi kwa wanafunzi wako?

# Somo la 3
# Jinsi ya kuwa meneja wa Mungu



**1. Kweli Kuu ya Kibiblia**

Kama meneja wa Mungu, ninapaswa kujitahidi kwa kila kitu ninachofanya.

**2. Mstari mkuu: Waroma 12:11 (Biblia Takatifu (SUV)**

Kwa bidii, si walegevu; mkiwa na juhudi katika roho zenu; mkimtumikia Bwana.

**3. Mafundisho ya mwanafunzi yaliyotumiwa katika somo hili**

Sura ya 3 ya Mwongozo wa Mwanafunzi inaenda pamoja na somo hili. Zoezi la 3 Mwongozo wa Somo, "Meneja wa Mungu," pia litatumika katika somo hili.

**4. Zoezi la utangulizi wa somo (dakika 5-7)**

Anza darasa kwa mojawapo wa mazoezi yaliyoorodheshwa hapa chini - kwa kumhoji mtu (Zoezi A) au mwanafunzi mmoja au wawili kuigiza mchezo wa kisasa wa "Lulu ya thamani kuu" (Zoezi B)

Kulingana na jinsi ulivyopanga kipindi hiki cha darasa, unaweza kutumia mazoezi yote haya katika kipindi cha darasa la leo. Kwa mfano, kwa kuanza darasa kwa zoezi moja, na kutumia mfano mwingine kwa wakati ufaao baadaye katika kipindi kijacho cha darasa.

**A. Mahojiano na Meneja Mkristo**

Anza darasa kwa kumhoji mtu ambaye amewahi au kwa sasa anafanya kazi kama meneja katika biashara. Kuna njia mbili ambazo unaweza kuzingatia kwenye mahojiano haya.

Njia moja—uliza ikiwa kuna mwanafunzi wako ambaye ameshafanya kazi kama meneja katika biashara. Mchague atakayejitolea ili aje mbele darasani, na umhoji mtu huyo, ukitumia maswali yafuatayo hapa chini. Ili kuhakikisha kuwa kuna mtu kama huyo, itakuwa vizuri kumtambua mtu huyu kabla ya kipindi cha darasa la leo kuanza.

Njia ya pili—panga mapema mtu ambaye kwa sasa ni au amewahi kufanya kazi kama meneja katika biashara. Mwambie mtu huyo aje darasani na umhoji, au urekodi video ya mahojiano kati yako naye na uichezekwa darasa lako.

**Maswali ya mahojiano yanayopendekezwa:**

1. Umeajiriwa wapi kama meneja, na umefanya kazi kama meneja kwa muda gani?
2. Ni tajriba gani iliyohitajika kabla ya kupata nafasi hiyo ya kuwa meneja?
3. Je, unawasimamia watu wangapi?

4. Je, ni tofauti gani kuu iliyoko kati ya majukumu yako kazini na kazi ya wale walio chini ya usimamizi wako?
5. Je, ni tofauti gani kuu iliyoko kati yako wewe kama meneja na mmiliki wa biashara yako?
6. Je, uhusiano kati yako na mmiliki ukoje?
7. Je, ni fursa gani uliyo nayo ya kuwa na uhusiano na Yesu kama meneja katika biashara yako?

**B. Mchezo wa kuigiza: Lulu ya thamani kuu.**

Chagua wanafunzi 2 kusoma huu kama mchezo wa kuigiza.

Toleo la kisasa la mfano wa Kristo wa "Lulu ya Thamani Kuu."

Mistari ya **Mnunuzi** iko katika ***italiki*** na **ya muuzaji** ni ya kawaida.

*"Nataka lulu hii. Ni bei gani?"*

"Kwa kweli," muuzaji anasema, "ni ghali mno."

*"Hata hivyo, tunauliza ni kiasi gani?"*

"Kiasi kikubwa sana."

*"Je, unafikiri ninaweza kuinunua?"*

"Ah, bila shaka, kila mtu anaweza kununua."

*"Lakini, si ulisema ni bei ghali mno?"*

"Ndio."

*"Sawa, ni bei gani?"*

"Kila kitu ulicho nacho," anasema muuzaji

Tumeamua, *tunasema "Sawa, nitainunua."*

*"Kweli, nina elfu kumi kwenye benki."*

"Vizuri — dola elfu kumi. Na nini kingine?"

*"Ni hayo tu. Hitu ndizo pesa nilizonazo.""Hata hivyo, nina dola chache mfukoni."*

"Ngapi?"

Tunaanza kutafuta. *"Hebu angalia – thelathini, arobaini, sitini, themanini, mia, dola mia moja ishirini."*

"Ni sawa. Una nini kingine?"

*"Kwa kweli, hakuna kitu kingine. Ni hizo tu."*

"Unaishi wapi?" Bado anachunguza.

*"Katika nyumba yangu. Ndio nina nyumba."*

"Nyumba pia." Anaandika.

*"Unamaanisha nitaiishi kwenye kambi yangu?"*

"Una kambi? Hiyo, pia. Nini kingine?"

*"Nitalala kwenye gari langu!"*

"Una gari?"

*"Mawili."*

"Yote yanakuwa yangu, magari yote mawili. Nini kingine?"

*"Kweli, tayari unazo pesa zangu, nyumba yangu, kambi yangu, na magari yangu. Unataka nini zaidi?"*

"Je, unaishi peke yako katika ulimwengu huu?"

*"Hapana, nina mke na watoto wawili…."*

"Ah, ndio, mke wako na watoto pia. Nini kingine?"

*"Sina kilichobaki! Nimebaki peke yangu sasa."*

Ghafla muuzaji anashangaa, "Loo, karibu nilisahau! Wewe pia! Kila kitu kinakuwa changu — mke, watoto, nyumba, pesa, magari — na wewe pia." Kisha anaendelea. "Sasa sikiliza — nitakuruhusu utumie vitu hivi vyote kwa sasa. Lakini usisahau kwamba vyote ni vyangu, kama wewe ulivyo. Na kila ninapohitaji chochote lazima unipe, kwa sababu sasa mimi ndiye mmiliki."

Kutoka kwa *Disciple,* na Juan Carlos Ortiz, (Wheaton, IL: Creation House, 1975) uk 34-35, kama ilivyonukuliwa katika *Improving Your Serve*, na Charles R. Swindoll, uk 35-36.

**5. Jadili Hoja A, "Meneja ni nini?"**
**(Dakika 5-10 Mwongozo wa Mwanafunzi ukurasa wa 13)**

Tanguliza mada ya leo kwa kujadili ya Hoja A, "Meneja ni nini?" Mwishoni mwa darasa la leo tutahakikisha wanafunzi wetu wanaelewa maana kuwa meneja wa Mungu. Lakini hata kati ya Wakristo, hili si jambo la kawaida la kuzungumzia uhusiano wao na Mungu. Mara nyingi tunasikia juu ya umuhimu wa kumtii Mungu, na kumpenda Mungu, n.k.

Kwa hivyo tunapozungumza kuhusu kuwa meneja wa Mungu, tunajaribu kuwaambia wanafunzi wetu nini? Tunataka waone tofauti kati ya wamiliki na mameneja, na wasijione kama wamiliki wa kile walicho nacho, mbali wasimamizi wa kile Mungu amewapa. Yote ni masuala ya mtazamo, na ya tabia.

Taja kwamba kuwa Mkristo ni zaidi ya kumwambia Yesu atusamehe dhambi zetu. Mungu anatarajia mengi kutoka kwetu zaidi ya kwenda kanisani Jumapili kwa maisha yetu yote. Tuna jukumu la kumtumikia Yesu siku 7 kwa wiki.

Kuwa Mkristo inamaanisha kuwa nimempa Yesu maisha yangu. Yeye sasa ni mmiliki wangu na Bwana wangu— na sasa namfanyia kazi. Amenipa jukumu la kuwa msimamizi Wake kwa vitu vyote alivyonikabidhi.

Katika ulimwengu wa biashara, meneja ni meneja tu akiwa “kazini mahali pake pa ajira.” Mtu huyu anapoenda nyumbani, ana majukumu mengine- kama mzazi, mume, mke, kaka, dada, n.k. Lakini kuwa meneja wa Mungu ni 24-7. Siku zote tuko “kazini” paoja na Mungu — siku zote tuna jukumu la kuwa wasimamizi wazuri wa kazi ya Mungu.



**6. Jadili Hoja B, “Je, Mungu amenipa wajibu wa kusimamia nini?”
(Dakika 7-10 Mwongozo wa Mwanafunzi ukurasa wa 13-14)**

Jadili kwa kifupi kile Mungu ametupatia kusimamia. Epuka kuingia kwenye majadiliano marefu ya kina kuhusu jinsi ya kuwa meneja mzuri wa Mungu kwa mada hizi. Tutalenga haya kwa majadiliano yetu kwenye Hoja D, “Ninawezaje kuonyesha kuwa mimi ni meneja wa Mungu?”

## B. Je, Mungu amenipa wajibu wa kusimamia nini?

1. Wakati
2. Pesa
3. Karama za Roho Mtakatifu
4. Jamii na mahusiano
5. Kazi

*Imenukuliwa kutoka kwa Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 13-14*

Tunachotaka wanafunzi wetu kufahamu wakati huu ni “majukumu” maalum kwenye sehemu tofauti za maisha yao ambayo Mungu anataka wazione kama majukumu kutoka kwa Mungu. Wanapaswa kujiona kama mameneja wa Mungu katika kila sehemu.

Unaweza kuandika orodha zaidi ya ile iliyotolewa kwenye Mwongozo wa Mwanafunzi. Unaweza kuandika orodha hii kwenye karatasi kubwa na uiweke ukutani mwa darasa lako na uirejee unapoendelea na kipindi cha darasa.

Wahimize kuzingatia jinsi wanavyoweza kuwa mameneja wazuri wa Mungu hivi sasa wakiwa darasani. Waambie waeleze jinsi wanavyoweza kufanya hivyo.

Je, utajuaje kile Mungu anataka usimamie? Atakwambia. Anayaita haya majukumu. Majukumu ni sheria, vitu ambavyo umepewa kufanya, vitu ambavyo lazima uvifanye.

Uhuru au nafasi ni kitu ambacho umepewa, lakini sio lazima ufanye ikiwa hutaki. Kwa mfano, uko huru kuandika barua nyumbani kwa wazazi wako, au kuwapigia simu. Lakini majukumu ni tofauti.

Je, ni jukumu gani kubwa ambalo Mungu anakupa? Kumpenda Mungu (Marko 12:30). Angalia jukumu lako ni nini. Ni kupenda. Angalia linahusiana zaidi na nani – Mungu. Wajibu wako mkuu sio kujipenda wewe mwenyewe au kuwapenda wengine, ni kumpenda Mungu.

Kama mwanafunzi, ni jukumu gani Mungu amekupa? Swali moja linalokukabili ni, "Nifanye nini ili kujifunza?" Majibu yanayopendekezwa yanaweza kuwa:



Kuwa makini

Kusikiliza

Kushiriki darasani

Kuuliza maswali

Kuandika

Kusoma (nje ya darasa)

Kupitia tena

Kuhusisha mafundisho ya kibiblia na maisha yako

Waulize wanafunzi wako jinsi wanaweza kumwonyesha Mungu wanampenda kwa kusikiliza darasani. Waache wasikilize kwa makini darasani kwa dakika moja na kisha uwaeleze walichofanya. Wamesikiliza na kuonyesha upendo wao kwa Mungu.

Unaweza kufikiria haraka kuliko watu wanavyosema. Kwa hivyo unaposikiliza darasani unaweza pia kufikiria zaidi ya maneno waliyoyasema. Mawazo ya ziada unayoyawaza yanaweza kuonyesha upendo kwa Mungu.

Unawezaje kufungamanisha usikilizaji na kumpenda Mungu?

"Usiwe na akili yenye uvivu" (Warumi 12:11).

"Kazi yoyote unayoifanya, ifanye kwa moyo wako wote" (Wakolosai 3:23 NLB).

Kufikiria ni kazi. Kufikiria kunajumuisha kufanyisha ubongo kazi.

Kusikiliza kunaweza kukosa matendo. Unaweza kukaa na kupokea maneno kupitia kwa masikio yako. Lakini ikiwa kusikiliza kutakusaidia kuonyesha upendo wako kwa Mungu, lazima kuwe kwa matendo.

Njia moja bora ya kutumia akili yako wakati unasikiliza darasani ni kufikiria jinsi unavyoweza kutumia yale unayofundishwa (ambayo ni kutekeleza). Unawezaje kuyatumia katika uhusiano wako na Mungu? Pia unawezaje kutumia kile unachofundishwa katika uhusiano wako na wanafunzi wengine?

Jambo moja ambalo litasaidia ni kuandika maoni ya matumizi kibinafsi unapofikiria! Cha muhimu kinapaswa kuwa kutafuta njia za kutumia kibinafsi mistari inayotumiwa darasani. Ubora wa usikilizaji wako ni njia moja kuu ya kujifunza kitu cha maana darasani.

Sikiliza kwa hamu — angalia 2 Wakorintho 8:11, Biblia Habari Njema.

3

**7. Jadili Hoja C, "Ni nini humfanya mtu kuwa meneja mzuri wa Mungu?" (Dakika 10-15 Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 15-16)**

Jadili sifa 6 zilizoorodheshwa katika Mwongozo wa Mwanafunzi ambazo zinaeleza ni nini kinachomfanya mtu kuwa meneja mzuri wa Mungu. Unaweza kuunganisha haya kwa kile kilichosemwa katika mahojiano mwanzoni mwa kipindi hiki cha darasa. Je, sifa hizi za meneja mzuri wa Mungu zinalingana au zinatofautiana kivipi na zile za meneja mzuri katika biashara?

## C. Ni nini hufanya mtu kuwa meneja mzuri kwa niaba ya Mungu?

1. Ukuaji uliosawazishwa
2. Meneja mzuri hujifunza (kukasimu) kukabidhi majukumu
3. Mmiliki wangu ni nani – Je, kiongozi wangu ni nani? Ni Mungu!
4. Upendo ni sehemu kubwa sana ya kuwa meneja mzuri zaidi wa Mungu
5. Uaminifu
6. Utiifu

*Orodha imechukuliwa kutoka kwa ukurasa wa 15-16 Mwongozo wa Mwanafunzi*

Baada ya kujadili sifa hizi sita za meneja mzuri wa Mungu, unaweza kuwapa wanafunzi wako fursa ya kujadili majibu yao kwa **swali la 10 kwenye Zoezi 3 la Mwongozo wa Somo, "Meneja wa Mungu."**

**Swali la 10. Soma simulizi katika Luka 12: 42-48. Ni mambo gani yaliyomfanya bwana kupendezwa na kazi ya mtumishi mwema?**

**8. Jadili Hoja D, "Ninawezaje kuonyesha kuwa mimi ni meneja wa Mungu?" (Dakika 7-10 Mwongozo wa Mwanafunzi ukurasa wa 16-17)**

Sehemu hii inatuelekeza kwa matumizi kibinafsi. Lengo letu hapa ni kuwafanya wanafunzi kuanza kubinafsisha fursa ambazo Mungu anaweka mbele yao leo. Ni maswala 3 tu yanayoshughulikiwa hapa — wakati wangu, kazi yangu, na mali zangu.

Hoja hii inahusiana na Hoja B, "Je, Mungu amenipa wajibu wa kusimamia nini?" ambayo iliorodhesha maswala mengine pia. Pengine hautakuwa muda wa kujadili kwa kina sehemu hizi zote, lakini waelekeze kufikiria kwa makini kila sehemu na waweke malengo maalum ya jinsi wanavyoweza kuwa mameneja wazuri wa Mungu.

Hakikisha umeunganisha maswala yote ambayo tumezungumzia leo, na uwafanye waone kile wanachoweza kuanza kufanya leo ili kuwa meneja mzuri wa Mungu.

Kwa kujadili mada ya "Wakati wangu," pinga kauli ya kawaida ya "Laiti ningalikuwa na wakati zaidi, ningalifanya mengi zaidi."

Wakati zaidi haungesaidia. Angekuwa na wakati zaidi wa kusimamia, lakini je, matumizi ya wakati yangekuwa bora zaidi? Kanuni ya Mungu ni kwamba – ikiwa wewe ni mwaminifu kwa kidogo, basi atakupa zaidi.

Wakati wako — unawezaje kutumia wakati wako vizuri? Panga wakati kwa mambo muhimu zaidi.

**Waefeso 5:16, Biblia Takatifu (SUV)**

**Mkiukomboa wakati kwa maana zamani hizi ni za uovu.**



Katika kujadili mada ya "kazi," onyesha kwamba wanaweza kuanza kutumia jambo hili kwa maisha yao hata kama hawana kazi. Wanaweza kuitumia kwa kazi za nyumbani ambazo wanapaswa kufanya mahali wanapoishi. Au wanaweza kuitumia kwa kiwango cha kibinafsi katika kazi za kujitolea.

**9. Jadili Hoja E, "Mtazamo wangu unaonyesha ikiwa ninafanya kazi kama meneja kwa niaba ya Mungu." (Dakika 5 Mwongozo wa Mwanafunzi ukurasa wa 18)**

Wasaidie wanafunzi wako kuona kwamba mitazamo wanayoendeleza leo itaathiri maisha yao yote. Kuwa meneja wa Mungu ndio msingi wa suala la mtazamo. Mifumo yao ya kufikiria itachangia mafanikio yao kuifanya hii kuwa sehemu yenye mafanikio maishani mwao.

Mtazamo wako ni muhimu kuonyesha ikiwa unafanya mambo kama meneja wa Mungu.

Jadili Warumi 12:11 na Wakolosai 3:23 na jinsi aya hizi zinahusiana na mitazamo yako. Onyesha kwamba mara nyingi ubinafsi wetu unaweza kuwa kikwazo kikubwa zaidi kwa kazi yetu kwa Bwana.

**10. Jadili Hoja F, "Matokeo ya kuwa meneja wa Mungu."**
**(Dakika 5 Mwongozo wa Mwanafunzi ukurasa wa 19)**

Pengine umeshughulikia suala hili katika kipindi cha darasa la leo. Tumia hatua hii kukusanya mambo muhimu yaliyofunikwa katika somo hili la leo. Wasaidie kuona nguvu ya kujifunza jinsi ya kuwa meneja mzuri wa Mungu — Atakupa majukumu zaidi. Njia nzuri ya kuona fursa inakujia ni kuwa waaminifu mahali ambapo Mungu amekuweka leo.

**11. Maombi ya kibinafsi (dakika 10)**

**A. Kuwa "Meneja wa Mungu" darasani**

Angazia matumizi binafsi ya kuwa meneja wa Mungu darasani. Pitia mambo ambayo Mungu amewapa kusimamia ambayo yanahusiana moja kwa moja na wakati huu wa darasa. Toa mifano inayoonyesha haya. Waache wanafunzi waandike jambo moja ambalo wanaweza kufanya katika kipindi kitakachofuata cha darasa ambalo litaonyesha kuwa wao ni mameneja wazuri wa Mungu.

Pia wahimize kuangazia sehemu zingine za maisha yao ya kila siku ambapo wanataka kujaribu kuwa mameneja wazuri wa Mungu. Waambie waweke malengo kwa yale wanayoweza kufanya katika siku 2 zijazo ili kuanza kuwa meneja mzuri wa Mungu katika sehemu hii.

**B. Kuwa "Meneja wa Mungu" hata na pesa zako**



Ikiwa wanafunzi wako wana mapato kwa sasa, wahimize kutoa angalau 10% kama zaka kwa Mungu.

**12. Kazi**

A. Wape maswali kutoka 2 Wakorintho 9:7 mwishoni mwa kipindi cha darasa.

B. Sahihisha Zoezi la 2 la Mwongozo wa Somo "Ushuhuda wangu," na Zoezi la 3, "Meneja wa Mungu."

C. Waache wanafunzi wako wasome Sura ya 4 kutoka kwa Mwongozo wa Mwanafunzi ili kujiandaa kwa kipindi kifuatacho cha darasa.

D. Wape Zoezi la 5 la Mwongozo wa Somo, "Kazi yangu," ili kufuata mazungumzo ya darasa letu la leo. Wahimize kutafuta fursa za kutumia wakati wao wa kazi kama fursa ya kufanyisha kazi yale ambayo tumejadili leo.

**13. Tathmini na maoni yangu ya kufundisha somo hili wakati ujao.**

Tafadhali orodhesha maoni yako kuhusu oboreshaji wa somo hili.
Ni sehemu zipi zilifanya kazi bora zaidi?
Ni sehemu zipi zilikuwa gumu zaidi kwa wanafunzi kuelewa?
Ni nini kilionekena kuwa cha msaada zaidi kwa wanafunzi wako?

# Somo la 4
# Ushirika

**1. Kweli kuu ya Kibiblia**

Huduma ya ushirika inakuwa huduma kwa ukuaji wakati ninatafakari sababu za Mungu za kuwa na huduma hii.

**2. Mstari mkuu:**



Matendo 2:42 (Biblia Takatifu (SUV)

Wakawa wakidumu katika fundisho la mitume, na katika ushirika, na katika kuumega mkate, na katika kusali.

**3. Mafundisho ya mwanafunzi yaliyotumiwa katika somo hili**

Sura ya 4 katika Mwongozo wa Mwanafunzi inaendana na somo hili.

**4. Zoezi la utangulizi wa somo**

Unahitaji "ndoano" nzuri kwa somo hili. La sivyo, somo hili linaweza kuwachosha sana wanafunzi na kuwafanya kutovutiwa nalo. Njia mbili zimeorodheshwa hapa chini.

**A. Video ya Mateso ya Kristo (*Passion of Christ)***

Kwa kuwa lengo kuu la somo hili linahusu maana ya kifo cha Kristo, unaweza kuanza kipindi chako cha darasa kwa kuonyesha sehemu ulizo chaguwa kutoka kwa sinema, Mateso ya Kristo (*The Passion of Christ).* Sehemu moja ambayo kwa kweli inaonyesha maumivu ambayo Yesu alipata kwa ajili yetu ni pale anapopigwa.

Njia nyingine ni kuwaonyesha wanafunzi wako sinema nzima siku moja kabla ya kipindi hiki cha darasa.

**B. Kuwasilisha kwa kutumia 'PowerPoint' kuhusu ushirika**

Unaweza kuandaa mawasilisho ya PowerPoint inayoonyesha mambo kadha wa kadha kuhusu ushirika. Ikiwa utaandaa PowerPoint, itabidi uamue ikiwa utaitumia kama "kichangamshi katika somo," au ikiwa utaitumia unapofundisha sehemu zingine za somo hili. Unaweza:

1. Kuonyesha picha ya ibada ya ushirika wa kanisa la kisasa.

2. Kuonyesha picha ya watoto wanaoshiriki katika ibada ya ushirika na uwaulize wanafunzi wako wazungumzie kumbukumbu za mara yao ya kwanza kushiriki katika ibada ya ushirika.

3. Kuonyesha picha ya mikono ya Yesu iliyochanwa na kutokwa na damu.

**5. Jadili Hoja A, “Je, Ushirika Mtakatifu” unamaanisha nini? (Dakika 5 Mwongozo wa Mwanafunzi ukurasa wa 20)**

Anza majadiliano yako darasani kwa kuwauliza wanafunzi wako wafafanue neno “ushirika.” Orodhesha majibu yao ubaoni — wanaweza kutoa fafanuzi kadhaa ambazo ni tofauti — hilo ni sawa.

Baada kuorodhesha fafanuzi zao, onyesha matumizi yake maalum kulingana na ibaada ya kanisa. Katika Mwongozo wa Mwanafunzi kwenye ukurasa wa 20 kuna orodha ya maneno kadhaa ambayo hutumiwa kueleza ibaada maalum ya kanisa. Onyesha kuwa makanisa mbalimbali hutumia majina tofauti, na pia yana mitindo mbalimbali ya kusherehekea ibaada hii maalum.

Usiwache mjadala huu uwe wa kujaribu kueleza mitindo mbalimbali ya makanisa. Eleza tu kwamba ni tofauti, na itakuwa sawa.

Pia eleza kuwa neno “ushirika” lina ufafanuzi wa jumla ambao ni “kushiriki.” Eleza kuwa ufafanuzi huu una sehemu muhimu katika kutusaidia kuelewa madhumuni ya ibaada hii maalum ya kanisa — tutajadili suala hili kwa undani zaidi baadaye katika kipindi cha darasa la leo.

Epuka kuingilia mjadala wa ikiwa mkate na divai hubadilika kuwa damu na mwili wa Yesu au la. Suala hilo silo lengo la somo letu leo — na si suala kuu la Wakristo wapya. Rejelea kweli kuu ya kibiblia kwa kusudi la somo hili.

**6. Jadili Hoja B, “Ni vitu gani maalum vinavyotumika katika ibada ya ushirika mtakatifu?” (Dakika 3-5 Mwongozo wa Mwanafunzi ukurasa wa 20)**

Eleza jinsi ibaada ya ushirika ilivyotofauti na ibaada zingine nyingi za kanisa. Inatumia chakula kama sehemu kuu ya ibaada.

Waeleze wanafunzi kuwa mara ya kwanza kabisa ya Yesu kuwaeleza wanafunzi wake kuhusu haya ilikuwa kabla tu ya kifo chake. Yesu na wanafunzi wake walikuwa wakisherehekea “Pasaka” siku maalum ya ukumbusho katika dini ya Kiyahudi. Pasaka ilikuwa chakula maalum ambacho kilitumika kukumbuka jinsi Mungu alivyowalinda Wayahudi usiku ambao malaika wa mauti alipitia Misri na kuwaua watoto wa kwanza kwa kila nyumba. Hii ilikuwa siku takatifu zaidi kwa Wayahudi katika siku za Yesu na ilijumuisha chakula kamili, na kila sehemu ya chakula ilikuwa na ishara maalum ya kiroho.

Yesu hakuleta maana mpya kwa tamaduni za muda mrefu za Kiyahudi. Alichukua vyakula viwili vya kawaida vya siku hiyo — mkate na divai — na akaleta maana mpya kwao.

Yesu pia aliwaamuru wanafunzi wake wafanye hivi kama njia ya kumkumbuka kile alichowafanyia. Tazama Luka 22:7-23.

Yesu aliwaambia kwamba mkate huo ni ishara ya mwili Wake uliotolewa kwa ajili yao — kwa ajili ya wokovu wetu. Tazama Luka 22:19.

Yesu alisema divai hiyo ilikuwa ishara ya damu yake — ndiyo maisha yake — ambayo Alitoa kwa ajili ya wokovu wetu. Tazama Luka 22:20.

Ishara hizo hizo zinaelezwa kwa kanisa la Korintho wakati Paulo anatoa maagizo jinsi ya kufanya ibada ya ushirika. Tazama 1 Wakorintho 11:17-34. Andiko hili litaangaziwa pakubwa katika majadiliano katika kipindi chote cha darasa la leo.

**7. Jadili Hoja C, "Kwa nini tunatumia mkate na divai katika ibada ya ushirika mtakatifu?" (Dakika 5 Mwongozo wa Mwanafunzi ukurasa wa 21)**

Waeleze wanafunzi wako kwamba viongozi wa dini hawakufanya uamuzi wa kutumia mkate na divai—Yesu mwenyewe alitoa maagizo haya. Na Mungu alikuwa ametoa maagizo maalum kuhusu jinsi chakula cha Pasaka kitasherehekewa wakati wa Agano la Kale.

4

Mkate na divai ni ishara zinazoonekana ambazo tunaweza kugusa, kuonja, na kula kama ukumbusho wa kile Yesu alitufanyia. Yesu alitaka kuhakikisha kuwa hatusahau dhabihu kubwa ambayo Alitoa kwa ajili yetu.

Ikiwa haukutumia sinema ya Mateso ya Kristo (*The Passion of Christ)* kama kisisimuzi katika somo, unaweza kutumia wakati huu darasani kuwaonyesha wanafunzi wako sehemu ulizochagua katika sinema hiyo. Sehemu ambazo zinaonyesha mapigo ya Yesu kwa ajili yetu zinapendekezwa. Picha hii inaweza kusaidia kuona ukweli wa maana ya ibaada ya ushirika. Ikiwa ulitumia video hii mwanzoni mwa kipindia chako cha darasa, unaweza kurejelea yale waliyoyaona mwanzoni mwa kipindi cha darasa.

**8. Jadili Hoja D, "Je, kusudi la ushirika mtakatatifu ni nini?" (Dakika 15 -20 Mwongozo wa Mwanafunzi ukurasa wa 21)**

Tumia muda wa kutosha darasani kujadili ni kwa nini tuna ushirika.
Wambie wanafunzi wako wasome 1 Wakorintho 11:23-34 ili kuona hoja tano ambazo zinaelaza ni kwa nini tuna ibaada hii. Angalia ukurasa 21 wa Mwongozo wa Mwanafunzi kwa maelezo haya.

## D. Kusudi la ushirika Mtakatifu ni nini?

1. Kumwabudu Mungu. (1 Wakorintho 11:24-26)
2. Kukumbuka kuwa Yesu alikufa kwa ajili yetu. (1 Wakorintho 11:24-25)
3. Kutukumbusha kutarajia kuja kwa Yesu tena. (1 Wakorintho 11:26)
4. Kutupatia fursa ya kujichunguza moyoni (kuchunguza maisha yetu). (1 Wakorintho 11:27-32)
   a. Tunaweza kuungama dhambi zetu kwa Mungu.
   b. Tunaweza kuona ikiwa tumefikia malengo yetu.
5. Kutusaidia kutazama uhusiano wetu na wengine. (1 Wakorintho 11:29)
   a. Tunaweza kuomba msamaha ikiwa tumemkosea au kumuumiza mtu.
   b. Tunaweza kumtia mtu moyo.
   c. Tunaweza kuwashukuru wengine kwa kitu ambacho wamefanya.

*Imenukuliwa kutoka kwa Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa 21*

Wakati unajadili hoja ya 4, zungumzia dhambi katika maisha yetu na ushirika. Tunapaswa kuwa waangalifu ili tusigeuze huu kuwa majadala wa teolojia ya Kanisa. Makanisa mengi yanaamini kwamba ushirika hauondoi dhambi yako. Ni picha ya kile Yesu amefanya kwa dhambi zetu.

Kama vile ubatizo wa maji hauoshi dhambi zako, pia ushirika haufanyi hivyo.

Sisitiza sababu ya Yesu kuanzisha desturi hii ya kidini.

Kuna jambo lingine linalowatatiza watu wengine-Itakuwaje ikiwa watu ambao si Wakristo watashiriki ushirika? Hata Wakristo wengine wanaogopa kushiriki ushirika kwa njia ambayo inaweza kuleta hukumu ya Mungu juu yao.

Sehemu ya mwisho ya 1 Wakorintho 11 inazungumzia matatizo katika kanisa la Korintho. Lakini ukweli juu ya ushirika ni kuwa-ikiwa wewe ni Mkristo, basi hii inaweza kuwa njia nzuri ya kuonyesha kuwa unampenda Mungu. Ikiwa wewe si Mkristo, basi kushiriki katika ushirika hakutakusamehe dhambi zako.
Bado utakuwa mwenye dhambi vile ulivyokuwa kabla ya kushiriki ushirika.

Sisitiza kwamba wokovu na msamaha wa dhambi huja kwa kutubu dhambi kwa Yesu. Yeye hutuosha kutoka kwa dhambi zetu, si chochote tunachofanya-ushirika au ubatizo wa maji au kwenda kanisani kitatufanyia hivyo.

Jambo lingine muhimu kusisitiza katika sehemu hii ya darasa ni kwamba ushirika unatukumbusha umuhimu wa “mwili wa Kristo.” Hii haimaanishi mwili wake mwenyewe – bali ni picha ya watu ambao ni Wakristo.

**9. Matumizi Binafsi (dakika 5-10)**

Angazia matumizi Binafsi kwa sababu tano za ushirika.

1. Waambie wanafunzi waandike sababu hizi tano katika jalada la Biblia yao.
2. Wakumbushe kwamba wanapokuwa katika ibada ya ushirika katika kanisa lao, wanapaswa kupitia sababu hizi ili kupokea mengi kutoka kwa ibaada hiyo.
3. Fikiria sababu hizi kila wakati unapokuwa katika ibaada kanisani.

**10. Kazi**

A. Wape maswali kutoka Wakolosai 3:23 mwishoni mwa kipindi cha darasa.

B. Sahihisha Zoezi la 4 la Mwongozo wa Somo “2 Wakorintho 9:7,” na Zoezi la 5, “Kazi yangu.”

C. Waache wanafunzi wako wasome Sura ya 5 “Ubatizo kwa Maji” kutoka kwa Mwongozo wa Mwanafunzi ili kujiandaa kwa kipindi kifuatacho cha darasa.

**11. Tathmini ya somo.**

Tafadhali orodhesha maoni yako kuhusu oboreshaji wa somo hili.
Ni sehemu zipi zilifanya kazi bora zaidi?
Ni sehemu zipi zilikuwa gumu zaidi kwa wanafunzi kuelewa?
Ni nini kilionekena kuwa cha msaada zaidi kwa wanafunzi wako?

# Somo la 5
# Ubatizo kwa Maji



**1. Kweli kuu ya Kibiblia**

Kila Ibaada ya ubatizo wa maji inanipa nafasi ya kuangalia uhusiano wangu na Mungu.

**2. Mstari Mkuu:**

Warumi 6: 3 Biblia Takatifu (SUV)

Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake?

**3. Mafundisho ya mwanafunzi yaliyotumiwa katika somo hili**

Sura ya 5 katika Mwongozo wa Wanafunzi inaendapamoja na somo hili. Zoezi la 6 la Mwongozo wa Somo, "Ubatizo wa maji," pia litatumika katika somo hili.

**4. Zoezi la utangulizi wa somo (dakika 5)**

Unapoanza somo la leo, unaweza kumpa nafasi mwanafunzi 1 au 2 kuzungumzia wakati walibatizwa kwa maji na hili lilimaanisha nini kwao.

**5. Jadili kuhusu ubatizo kwa maji katika Agano Mpya (dakika 5)**

Anza kipindi cha darasa la leo kwa majadiliano mafupi ya ubatizo kwa maji katika Agano Jipya. Hii ilikuwa desturi ambayo ilifanywa na Yohana Mbatizaji hata kabla ya Yesu kuanza huduma Yake. Tazama Mathayo sura ya 3.

Mathayo 3:13-17 pia inajumuisha maelezo ya kubatizwa kwa Yesu kwa maji na Yohana.

Waambie wanafunzi wako wataje maana ya ubatizo wa maji kama ulivyoofanywa wakati wa huduma ya Yohana. Ikiwa majibu yao ni sahihi kwa kuonyesha ni kwa nini Yohana alikuwa akiwabatiza watu, basi nenda kwa hoja nyingine.

Sababu ya Yohana ya kubatiza watu ilikuwa ishara ya nje kwamba wamekuwa waumini na wafuasi wa Mungu.

**6. Jadili Hoja A, "Maana ya kiroho ya ubatizo wa maji."**
**(Dakika 20-25 Mwongozo wa Mwanafunzi ukurasa wa 22-24)**

Tumia muda zaidi wa kipindi cha darasa kujadili maana ya kiroho ya ubatizo wa maji. Kuna sababu 5 zilizotolewa katika Mwongozo wa Mwanafunzi. Tutatumia maandiko 2 kama msingi wa majadiliano haya—Warumi 6: 1-10 na Wagalatia 2:20.

Onyesha kwamba baada ya kifo na ufufuo wa Yesu, maana mpya ziliambatanishwa na ishara hii ya kidini. Eleza tofauti kati ya tendo la kiroho la wokovu na ishara ya kiroho ya wokovu -ubatizo wa maji.

Jadili kila moja ya hoja hizi 5, ukionyesha jinsi ubatizo wa maji ni ishara ya haya katika uhusiano wetu na Yesu.



## A. Maana ya kiroho ya ubatizo wa maji

1. Ninajitambulisha na Kristo katika kusulubiwa kwake. (Wagalatia 2:20, Warumi 6:6)
2. Ninajitambulisha na Kristo katika kifo chake. (Warumi 6:3)
3. Ninajitambulisha na Kristo katika kuzikwa kwake. (Warumi 6:4)
4. Ninajitambulisha na Kristo katika ufufuo wake. (Warumi 6:4-5)
5. Ninajitambulisha na Kristo katika njia yake mpya ya kuishi. (Wagalatia 2:20)

*Imenukuliwa kutoka kwa Mwongozo wa Mwanafunzi, kurasa za 22-24*

**7. Jadili Hoja B, "Ni kwa nini nibatizwe kwa maji?"**
**(Dakika 5 Mwongozo wa Mwanafunzi ukurasa wa 24)**

Hakikisha wanaelewa kuwa ubatizo wa maji ni ishara tu. Haiondoi dhambi zozote za binadamu. Hata hivyo, Biblia inatufundisha kwamba tunapaswa kubatizwa kwa maji baada ya kuwa Mkristo.

Kwa kifupi jadili hoja tatu zilizotolewa katika Mwongozo wa Mwanafunzi za kwanini wanapaswa kubatizwa kwa maji.

## B. Ni kwa nini nibatizwe kwa maji?

1. Ni njia moja ya kumtii Mungu. (Mathayo 28:10-20)
2. Ni ushuhuda kwa umma kwamba nimekuwa Mkristo.
3. Ni hatua nyingine katika ukuaji wangu wa kiroho.

*Imenukuliwa kutoka kwa Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 24*

**8. Jadili Hoja C, "Ni wakati gani nanapaswa kubatizwa kwa maji?" (Dakika 5 Mwongozo wa Mwanafunzi ukurasa wa 24)**

Elekeza majadiliano yako kwa hoja hii kuhusu yale Biblia inasema. Waache wanafunzi watazame na kusoma maandiko haya ambayo yanazungumzia ubatizo wa maji katika kanisa la kwanza - Matendo 2:38, 41; Matendo 8:37-38; na Matendo 19:4-5.

Eleza kwamba makanisa tofauti yana desturi tofauti wakati wanapo shughulikia suala hili. Makanisa mengine hubatiza watu siku hiyo hiyo wanayomba kuwa Wakristo. Wengine wanahitaji Wakristo wapya kupitia darasa maalum. Makanisa mengine yana mahitaji ya umri — mtu lazima awe amefikia umri fulani.

Makanisa mengine hufungamanisha ubatizo wa maji na ushirika wa kanisa — unapojiunga na kanisa unabatizwa kwa maji.

Sisitiza umuhimu wa ukweli wa ubatizo wa maji — ni ishara kwa umma kwamba mtu amekuwa Mkristo.



**9. Jadili Hoja D, "Matokeo ya ubatizo wa maji" (Dakika 5 Mwongozo wa Mwanafunzi ukurasa wa 25)**

Katika kujadili matokeo ya ubatizo wa maji, sisitiza tena kwamba ubatizo wa maji hauoshi dhambi zako-ni ishara ya mabadiliko ya kiroho ambayo tayari yamefanyika katika maisha yako.

Faida ya kimsingi tunayopata katika ubatizo wa maji ni kitendo chetu cha utiifu kuwasiliana hadharani kwamba tumempa Yesu maisha yetu.

Itakuwa nzuri kuelezea kwamba mara tu baada ya Yesu kubatizwa kwa maji kwamba alipitia kipindi cha siku 40 ambapo alikumbana na majaribu makali kutoka kwa Shetani. Hii inaweza kuwa sio kweli kwa kila Mkristo mpya leo, lakini hatupaswi kushangaa ikiwa tunakabiliwa na majaribu makubwa ya kutenda dhambi siku zifuatazo baada ya ubatizo wetu kwa maji.

Eleza kwa kifupi kwamba ubatizo wa maji haupaswi kuchanganywa na ubatizo wa Roho Mtakatifu-suala ambalo tutajadili kwa undani zaidi katika *Mafunzo ya Vikundi kwa Maisha Mapya* kozi ya **Maisha Ya Kikristo Yenye Mafanikio**.

**10. Matumizi Binafsi (dakika 5-10)**

Angazia matumizi binafsi kuhakikisha kuwa uhusiano wao na Mungu uko sawa. Uhusiano huu wa kiroho na Yesu ni muhimu zaidi kuliko tendo la ubatizo kwa maji.

Ikiwa mwanafunzi wako yeyote hajabatizwa kwa maji, unaweza kupanga kuwa na ibaada ya ubatizo wa maji ambayo inaweza kufuata hii.

**11. Kazi**

A. Sahihisha Zoezi la 6 la Mwongozo wa somo, “Ubatizo wa Maji.”

B. Waache wanafunzi wako wasome Sura ya 6, “Maombi,” kutoka kwa Mwongozo wa Mwanafunzi kujiandaa kwa kipindi kijacho cha darasa.

**12. Tathmini ya somo**

Tafadhali orodhesha maoni yako kuhusu oboreshaji wa somo hili.
Ni sehemu zipi zilifanya kazi bora zaidi?
Ni sehemu zipi zilikuwa gumu zaidi kwa wanafunzi kuelewa?
Ni nini kilionekena kuwa cha msaada zaidi kwa wanafunzi wako?

# Somo la 6
# Maombi

**1. Kweli kuu ya Kibiblia:**

Wakristo wanapaswa kufanya maombi kuwa sehemu ya maana ya kila siku.

**2. Mstari Mkuu:**

Wafilipi 4: 6 Biblia Takatifu (SUV)

Msijisumbue kwa neno lolote; bali katika kila neno kwa kusali na kuomba, pamoja na kushukuru, haja zenu na zijulikane na Mungu.

**3. Mafundisho ya mwanafunzi yaliyotumiwa katika somo hili**

Sura ya 6 katika Mwongozo wa Mwanafunzi inaenda pamoja na somo hili.



**4. Zoezi la utangulizi wa somo (dakika 5)**

**A. Maombi ya kuchekesha.**

Unaweza kuanza somo la leo kwa kusoma baadhi ya mifano ya maombi ya kuchekesha kutoka kwa watu. Kuna mifano mingi-watoto, Wakristo wapya, nk.

**B. Andika maombi kama shughuli ya kikundi kidogo.**

Waulize wanafunzi kukaa wawili wawili kisha uwaambie waandike maombi yao kwa Mungu. Wape hali maalum ambayo inaweza kuwa ya kawaida katika shughuli zao za kila siku, na wacha watumie hiyo kama lengo la maombi yao.

Baada ya kuandika maombi yao, waulize wanafunzi kadhaa wasome maombi yao darasani. Usifanye maamuzi ya  maombi gani ndiyo bora - badala yake tunataka kuwafanya wafikirie ni nini wanaweza kujumuisha katika maombi.

**5. Unaamua vipaumbele vyako leo**

Somo hili lina habari nyingi za kimsingi juu ya maombi. Utatathmini mahitaji ya wanafunzi wako ili kubaini ni masuala yapi utakayosisitiza zaidi wakati wa kipindi hiki cha darasa.

**6. Jadili Hoja A, “Maombi ni nini?”**
**(Dakika 5 Mwongozo wa Mwanafunzi ukurasa wa 26)**

Anza kipindi cha darasa la leo kwa kuwauliza wanafunzi wako kueleze maombi ni nini.

Sisitiza umuhimu wa kufanya maombi kuwa mawasiliano ya njia mbili. Wakristo wengi wapya wanaweza kuwa na wakati mgumu “kumsikiliza Mungu katika maombi yao,” hata hivyo wanapaswa kufahamu kuwa ni zaidi ya kumwambia Mungu kile ninachotaka na kisha kusema, “Amina.”

Mwongozo wa Mwanafunzi unatoa sababu mbalimbali za “Ninapaswa kuomba kwa nini?” Unaweza kuanza majadiliano haya kwa kuwauliza wanafunzi wako kujibu swali hili — Ninapaswa kuomba kwa nini?

Hoja ya tatu katika sehemu hii ni “Ni kwa nini ninaomba?” Tunataka kuliweka jambo hili liwe rahisi - tunamwomba Mungu. Wakristo wengi wapya huomba kwa Yesu — hivyo ni sawa — Yeye ni Mungu. Wengine huomba kwa Mungu Baba. Kusema kweli - Mungu hajishughulishi na maelezo haya — oh, unapaswa kuomba kwa Roho Mtakatifu ikiwa unataka ombi hilo lijibiwe.

Upendo wa Mungu ni wa ajabu — na Yeye anapenda kusikia tukiomba kwake. Hatakunja mikono yake mbinguni na kusema, “Sitajibu ombi hilo kwa sababu ulitumia maneno yasiyofaa.” Huyo siye Mungu tunayemtumikia.

**7. Jadili Hoja B, “Je, nitaombaje?”**
**(Dakika 5-10 Mwongozo wa Mwanafunzi ukurasa wa 27)**

Unaweza kuzungumzia sehemu hii haraka sana na kuendelea na maswala mengine kulingana na ukomavu wa kiroho wa wanafunzi wako. Lakini tusifikirie kwamba kila mtu anaelewa maswala haya.

Unapojadili hoja hizi 4, unapaswa kufahamu ni nini kitajadiliwa katika sehemu zingine za somo ili uweze kuahirisha maswali hayo kwa sehemu zinazofaa zaidi za somo.

Uweka mwelekeo kuwa wa vitendo na ulio rahisi. Tunataka kufanya maombi kuwa sehemu ya kawaida ya maisha yetu-kama vile kupumua.

Haswa kwa kueleza hoja ndogo - tumia lugha ya kawaida - wahimize wasiingie katika maswala ya mitindo ya dini. Unaweza kurejelea hadithi ambayo Yesu alisimulia juu ya wanaume wawili walioomba unapojadili hoja hizi nne. Tazama Luka 18: 9-14.

## B. Je, nitaombaje?

1. Tumia lugha ya kawaida
2. Mwambie Mungu ukweli
3. Omba jambo maalum – kwa uhakika
4. Jinsi mwili wako ulivyokaa sio jambo muhimu

*Imenukuliwa kutoka kwa Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa 27*

**8. Jadili Hoja C, "Napaswa kusema nini ninapoomba?"**
**(Dakika 5 -10 Mwongozo wa Mwanafunzi ukurasa wa 27-29)**

Hoja hii inashughulikia maswala ya kimsingi sana yanayohusiana na maombi. Tahadhari usifikirie kuwa kile kilicho dhahiri kwako kama Mkristo mkomavu ni dhahiri kwa wanafunzi wako.

Sisitiza umuhimu wa kufahamu kwamba sala ni zaidi ya kumwomba Mungu kile tunachotaka. Hoja nzuri ya kulinganisha ni kuwauliza wanafunzi wako kumfikiria rafiki na ni aina ipi ya mazungumzo wanayotaka kuwa nayo na rafiki huyo.

Je, ungehisi vipi ikiwa mtu huyu angezungumza nawe wakati anataka kitu kutoka kwako?

Je, ungehisi vipi ikiwa kila wakati mtu huyu alizungumza nawe, hakukuruhusu kusema chochote? Wanasema tu kile wanachotaka na kisha wanaondoka.

Unapopitia kila mojawapo wa hoja hizi — sisitiza kuhusu maswala ya vitendo ambayo yanahusiana na maisha yao ya kila siku, sio tu mikasa mikubwa ya maisha.



## C. Napaswa kusema nini ninapoomba?

1. Mwabudu Mungu
2. Muombe Mungu akusamehe dhambi zako. (Zaburi 66:2, Isaya 59:2)
3. Mshukuru Mungu (1 Wathesalonike 5:18)
4. Ombea kila kitu. (Wafilipi 4: 6)
5. Omba jinsi Roho Mtakatifu anavyokuongoza kuomba. (Waefeso 6:18)

*Imenukuliwa kutoka kwa Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 27-29*

**9. Jadili Hoja D, "Faida za kuomba ni zipi?"
(5 -7 dakika Mwongozo wa Mwanafunzi ukurasa wa 29-30)**

Jadili kwa haraka hoja hii ya somo. Mara nyingi Wakristo wapya hujitahidi kufanya maombi kuwa sehemu muhimu ya shughuli zao za kila siku. Faida hizi huja, sio kwa siku moja ya maombi, bali ni kwa vile wanavyozidi kufanya maombi kuwa sehemu ya kawaida yao ya kila siku.

## D. Faida za kuomba ni zipi?

1. Maombi hukusaidia kugundua mambo zaidi kuhusu Baba yako wa Mbinguni. (Mathayo 6: 9)
2. Maombi hukusaidia kupata msaada wa Mungu wakati wa shida. (Waebrania 4:16, 2 Wakorintho 12:7-10, Yakobo 1:2-8)
3. Maombi hukusaidia kupata amani na utulivu wa Mungu katikati ya shida. (Wafilipi 4:6-7)
4. Maombi hukusaidia kumpokea Roho Mtakatifu. (Matendo 2, Matendo 4:31, Luka 11:13)
5. Maombi hukusaidia kujua mapenzi ya Mungu kwa maisha yako. (Luka 22:41-43)
6. Maombi hukusaidia kuwa tayari kwa kurudi kwa Yesu. (Luka 21:36)

*Imenukuliwa kutoka kwa Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 29-30*

6

**10. Jadili Hoja E, "Ninawezaje kupata majibu ya maombi yangu?"
(Dakika 5 -10 Mwongozo wa Mwanafunzi ukurasa wa 31)**

Hii inaweza kuwa mojawapo ya jambo gumu kuelewa kwa Wakristo wapya. Wazo tu la kumwomba mtu ambaye huwezi kumwona ni jambo gumu kwa watu wengi. Lakini jambo kuu zaidi ni kusikia kutoka kwa Mungu — kupata majibu ya maombi yetu.

Tunapaswa kuwa waangalifu tunapofundisha kwamba hatuweki imani yetu kwa tajriba-hata tajriba nzuri. Tunapaswa kuwafundisha wanafunzi wetu kuangalia kile Mungu anasema katika Biblia-huo unapaswa kuwa msingi wetu wa kujibu swali hili.

Jadili kila hoja ndogo hapa. Hakikisha kuwa umeleta usawa kwa suala ambalo Wakristo wengine hawalielewi. Wengine wanaamini kwamba ikiwa unafanya mambo fulani basi umehakikishiwa kupata jibu unalotaka. "Ombeni kwa jina la Yesu. Tumia maneno fulani. Usiwe na shaka."

Maombi si fimbo ya kiinimacho ya kutumia kupata kile tunachotaka. Tunazungumza na Mungu wa ulimwengu huu wote, na anataka kusikia tunachosema.

Lakini tunaweza kupata mojawapo ya majibu 3 ya maombi yetu. Anaweza kusema "Ndio," "Hapana," au "Subiri kidogo." Jibu lolote atakalotoa — tunapaswa kulikubali.

## E. Ninawezaje kupata majibu ya maombi yangu?

1. Tarajia Mungu akujibu. (1 Yohana 5:14-15, Yakobo 1:6-7)
2. Pokea jibu la Mungu. (Mithali 28:9, 2 Wakorintho 12:7-10)

*Imenukuliwa kutoka kwa Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 31*

**11. Jadili Hoja F, "Kwa nini sipati majibu ya maombi yangu?"**
**(Dakika 5 -10 Mwongozo wa Mwanafunzi ukurasa wa 31-33)**

Sehemu hii ya somo la leo inaweza kuzua maswali mengi. Wengi wa wanafunzi wako bado wanaweza kuhangaika na suala hili.

Ni vyema kuwasaidia kujibu swali hili kulingana na kile Biblia inasema, sio tu kutokana na tajriba ya kibinafsi. Tunapaswa pia kuwasaidia kuona kwamba kwa sababu mtu mmoja alikuwa na jibu fulani haimaanishi tutakuwa na majibu sawa moja kwa moja.



Tafadhali kumbuka kuwa orodha ya vidokezo vidogo vilivyotolewa hapa sio sababu pekee za mtu kukosa majibu ya maombi. Wewe na wanafunzi wako mnaweza kuongeza maswala mengine muhimu ambayo yanatuzuia kupata majibu ya maombi yetu.

2 Samweli sura ya 21 inasimulia hadithi kutoka kwa maisha ya Mfalme Daudi ya kufahamu ni kwa nini hakupata majibu ya maombi yake, na jinsi alivyojaribu kusuluhisha tatizo hilo.

Jambo muhimu kusisitiza hapa ni kwamba Mungu husikia maombi yetu na anataka kutujibu. Mara nyingi kuna hali ambazo lazima tuzingatie ikiwa tutapata majibu ya maombi yetu. Lakini sio lazima tuwe wakamilifu kabla ya Mungu kujibu maombi yetu.

## F. Kwa nini sipati majibu ya maombi yangu?

1. Je, unamwuliza Mungu vitu visivyofaa? (Yakobo 4:14-15, Yakobo 4:3)
2. Je, umeshikilia dhambi maishani mwako? (Zaburi 66:18, Mithali 28:13)
3. Je, unakataa kumsikiliza Mungu? (Mithali 28:9)
4. Maombi mengine yana masharti. (1 Yohana 3:22-24)
5. Je, unaishi kwa shaka? (Waebrania 11:6, Yakobo 1:6-7)

*Imenukuliwa kutoka kwa Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 31-33*

**12. Jadili Hoja G, "Ninaomba lini?"**
**(Dakika 3-5 Mwongozo wa Mwanafunzi ukurasa wa 33-34)**

Hili ni jambo la msingi sana. Wahimize wanafunzi wako kutafuta fursa mbalmbali ambazo wanaweza kuomba-pamoja na wengine na wao wenyewe pia. Sisitiza umuhimu wa hija ndogo ya 2, **Kuwa na wakati uliotulia wa kuomba kila mara.**

## G. Nisali lini?

1. Kamwe usiache kuomba. (1 Wathesalonike 5:17)
2. Kuwa na wakati uliotulia wa kuomba kila mara.
3. Maombi ya kikundi.

*Imenukuliwa kutoka kwa Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 33-34*

6

**13. Jadili Hoja H, "Ni kwa nini maombi ni magumu?"**
**(Dakika 5 Mwongozo wa Mwanafunzi ukurasa wa 34-35)**

Suala hili pia linaweza kuwa changamoto kubwa kwa wanafunzi wako. Jambo muhimu la kusisitiza hapa ni kwamba hawapaswi kushangaa ikiwa sala ni ngumu. Tunaweza kuhitimisha kwa njia isiyofaa kuhusu jinsi sala linavyopaswa kuwa. Mara nyingi hitimisho hili haliambatani na kile Biblia inasema.

Kunaweza kuwa na maswala mengine ambayo wanafunzi wako wangeongeza kwenye orodha iliyotolewa katika Mwongozo wa Wanafunzi. JKuwa huru kuongeza maoni yao pia.

## H. Ni kwa nini maombi ni magumu?

1. Je, umemkasirikia Mungu? (Ayubu 21:15)
2. Je, unauhakika kwamba Mungu anasikia maombi yako? (Marko 11:24)
3. Je, unakabiliwa na shida nyingi katika maisha yako?
   (Luka 18:1, Yakobo 5:13)
4. Je, unakabiliwa na mateso? (Mathayo 5:44)

*Imenukuliwa kutoka kwa Mwongozo wa Wanafunzi, ukurasa wa 34-35*

**14. Matumizi binafsi (dakika 5-10)**

Unapohitimisha somo hili, wahimize wanafunzi wako kufanya maombi kuwa sehemu ya maisha yao ya kila siku. Sisitiza misingi ya maombi. Hata watoto wadogo wanaweza kuomba-kwa hivyo hatupaswi kufanya sala kuonekana kama sehemu ngumu ya maisha.

Wahimize wanafunzi wako kufanya maombi kuwa utaratibu wa kawaida kwa kila siku. Wahimize kuzingatia wazo la kuzungumza na Mungu kama Kiongozi wao juu ya kila hali wanayokabiliana nayo kwa siku nzima.

Unaweza kufunga darasa kwa kuwaambia wanafunzi wako wakiwa wawili kwa wawili waandike maombia, kwa kutumia habari ambayo tumejadili darasani leo. Unaweza kuwapa hali maalum ambayo ingekuwa ya kawaida kwa wanafunzi wako, na uwaombe waandike maombi yanayohusiana na suala hilo.

Baada ya kuandika maombi, wengine wanaweza kusoma maombi haya darasani.

**15. Kazi**

A. Sahihisha kazi ambayo haujakamilisha.

B. Waambie wanafunzi wako wajiandae kwa mitihani ambayo itatolewa wakati wa kipindi cha darasa litakalofuata.



**16. Tathmini ya somo**

Tafadhali orodhesha maoni yako kuhusu oboreshaji wa somo hili.
Ni sehemu zipi zilifanya kazi bora zaidi?
Ni sehemu zipi zilikuwa gumu zaidi kwa wanafunzi kuelewa?
Ni nini kilionekena kuwa cha msaada zaidi kwa wanafunzi wako?

# Somo la 7
# Mtihani

**1. Tanguliza kozi itakayojadiliwa.**

A. Wape Mwongozo wa Somo au Mazoezi yoyote ambayo yanapaswa kukamilishwa kabla ya kipindi cha kwanza cha kozi itakayofuata utakayofundisha.

B. Waelekeze wanafunzi kufungua ukurasa wa mwisho katika Mwongozo wa Somo Mpya. Wanapaswa kupata nakala safi ya ***Orodha ya Kazi za Darasani.*** Wape tarehe za majaribio ya chemsha bongo, Zoezi, na mtihani.

C. Wape Mwongozo wa Mwanafunzi mpya na uwaambie kurasa watakazosoma kabla ya kipindi kifuatacho darasani.

**2. Wape mitihani ya Somo hili.**

Kuna mitihaini miwili inayopatikana katika kozi hii. Tumia wowote unaodhani utakuwa wenye manufaa sana kwa wanafunzi wako.



**3. Ikiwa bado hujafanya hivyo, rudisha chemsha bongo zote na mazoezi ambayo umesahihisha.**

# Mwongozo wa Mwanafunzi

Mwongozo wa Mwanafunzi Haujajumuishwa kwenye hati hii,
lakini unapatikana katika hati tofauti.

Tafadhali angalia ukurasa wa 5 ya Mwongozo huu Wa Mwalimu kwa habari kuhusu matumizi ya Mwongozo wa Mwanafunzi.

# Mwongozo wa Somo

Haukujumuishwa kwenye hati hii, lakini unapatikana katika hati tofauti.

.

Tafadhali angalia ukurasa wa 5 ya Mwongozo huu Wa Mwalimu kwa habari kuhusu matumizi ya Mwongozo wa Somo.

# Mtihani

# Majibu ya mtihani

# Cheti cha Somo

Tazama ukurasa wa 5 wa mwongozo huu kwa habari zaidi kuhusu matumizi ya mtihani na cheti.

**Jina**______________________ **Kanuni za Kikristo**

**Tarehe**____________________ **Mtihani wa 1 Toleo la 5**

**Darasa**____________________ ________**Gredi**

**Maswali ya Kweli au Si Kweli** (alama 1 kwa kila moja)

Maagizo: Weka alama ___X___ iwapo jibu ni kweli.

Weka alama ___O___ iwapo jibu si kweli.

1.________Ushirika Mtakatifu na Meza ya Bwana ni kitu kimoja.

2.________Kabla ya watu kushiriki Ushirika Mtakatifu ni muhimu kwao kujiangalia ndani yao ili kuona kama wametenda dhambi.

3.________Mtu anakuwa Mkristo tu baada yake kubatizwa kwa maji.

4.________Unapoomba, unapaswa kumruhusu Mungu akuzungumzie.

5.________Mungu kamwe hataraji wewe ufanye kazi, kujitunza na kutunza familia yako.

6.________Mungu ameahidi kuwasaidia watu kwa mahitaji yao yote iwapo wao ni Wakristo.

7.________Unapaswa kuhubiri kila mara unapotoa ushuhuda wako.

8.________Kanisa la la mahali pamoja ni chombo cha Mungu cha kuwasaidia watu kuwa Wakristo imara.

9.________Ni sharti uwe Mkristo kwa muda usiopungua miaka 3 kabla ya kuanza kuwa meneja kwa niaba ya Mungu.

10._______Wakristo kamwe hawapaswi kutoa pesa kwa ajili ya kuwasaidia watu wasio Wakristo.

11._______Sababu ya pekee ya watu kwenda kanisani ni ili kwamba wawe Wakristo.

12._______Wakati unapotoa ushuhuda, daima unapaswa kutoa mfano mmoja kutoka kwa maisha yako ya kila siku ili kuonyesha Mungu anakusaidia kukua.

13._______Mungu daima atawapa watu kila kitu waombacho iwapo wanamwamini Mungu kwa dhati wanapoomba.

14._______Mungu hajali jinsi unavyotumia wakati wako iwapo wewe ni Mkristo.

15._______Sababu kuu ya kuwepo na kanisa la mahali pamoja ni kuwasaidia Wakristo kuzidi kukua na nguvu.

16._______Watu ni lazima daima wasimulie kuhusu maisha yao ya zamani ya dhambi kila mara wanapotoa ushuhuda kanisani.

**Maswali ya Kweli au Sio Kweli** ***Yameendelezwa***

17.______Mojawapo ya njia bora zaidi za Wakristo kukua ni kusemezana mmoja kwa mwingine na kuneneana kuhusu imani, matatizo na mafanikio.

18.______Iwapo Mkristo angependa kuwa meneja mzuri wa Mungu, yeye ni sharti ajifunze kuwa mwaminifu.

19.______Ukiwa katika ibada ya Ushirika Mtakatifu, unapaswa kuwaza kuhusu uhusiano wako na Wakristo wengine.

**Maswali ya Kuchagua Kati ya Majibu Mengi**

Chagua jibu sahihi na kisha uweke herufi ya chaguo lako kwenye pengo liloachwa. (Alama 2)

1.______Unapaswa kubatizwa kwa maji kwa sababu:
   A. ndipo utakuwa Mkristo.
   B. Yesu alikwambia ufanye hivyo.
   C. Musa alivuka Bahari ya Shamu ikiwa kama nchi kavu.

2.______Wakati watu wanaabudu Mungu, wao:
   A. Wanamwomba awasaidie katika maisha yao ya kila siku.
   B. Wanamwomba Mungu aponye mtu mgonjwa.
   C. Wanamwambia Mungu kile wanachopendezwa nacho kumhusu yeye (Mungu).

3.______Unapaswa kumtolea Mungu kwa sababu:
   A. inakubidi kufanya hivyo.
   B. unampenda Yeye.
   C. Usipotoa, huwezi kuwa Mkristo.

4.______Ni mara ngapi mtu anapaswa kuzungumza kuhusu maisha yake ya zamani katika dhambi wakati anapotoa ushuhuda kanisani?
   A. Kila mara anapotoa ushuhuda.
   B. Baadhi ya wakati mwingine.
   C. Hapaswi kamwe.

## Maswali ya Kulinganisha

Weka herufi sahihi kwa pengo linafaalo. (alama 3 kwa kila moja)

1.________Ushirika Mtakatifu

2.________Meneja kwa niaba ya Mungu.

3.________Ushuhuda

4.________Ubatizo wa Maji

5.________Kanisa la mahali pamoja

6.________Maombi

A. Unafanya hili mara moja pekee kuonyesha ya kuwa umekuwa Mkristo.

B. Kumkumbuka Yesu na kutazamia ujio wake mara nyingine tena.

C. Njia ya kuzungumza na Mungu.

D. Mungu anataka sisi tumpe Yeye asilimia 10% ya fedha za mapato yetu.

E. Inaonyesha kile ambacho Mungu anafanya katika maisha yako ya kila siku.

F. Kundi la watu wanaojumuika pamoja kwa ajili ya ushirika wa Kikristo.

## Maswali ya Majibu Mafupi

1. Katika ibada ya Ushirika Mtakatifu, mkate unawakilisha nini? (Alama 5)

   ________________________________________

2. Katika ibada ya Ushirika Mtakatifu, divai inawakilisha nini? (Alama 5)

   ________________________________________

3. Andika mistari ya kukariri hapa chini. (Alama 24)

   ________________________________________
   ________________________________________
   ________________________________________
   ________________________________________
   ________________________________________
   ________________________________________
   ________________________________________
   ________________________________________
   ________________________________________
   ________________________________________
   ________________________________________

**Maswali ya Majibu Mafupi** *Kuendelezwa*

4. Andika ushuhuda ukitumia miongozo minne iliyofunzwa katika darasa.
Iwapo unahitaji karatasi ya ziada, uliza mwalimu akupe.

Hakikisha umetoa mfano mmoja kutoka kwa eneo moja la maisha yako ya kawaida unaoonyesha jinsi Mungu anavyokusaidia kukua. Onyesha jinsi ulivyotumia mstari kutoka kwa Biblia kukusaidia kukua katika eneo hili la maisha yako ya kawaida. (Alama 21)

# Kanuni ya Kikristo

## Mtihani wa 1: Toleo la 5,
## Karatasi Ya Majibu Kwa Ajili Ya Mwalimu

### Ukurasa wa 1

**Maswali ya Kweli au Si Kweli**
(Alama 1 kwa kila moja)

1. X Kweli
2. X Kweli
3. O Si kweli
4. X Kweli
5. O Si Kweli
6. X Kweli
7. O Si Kweli
8. X Kweli
9. O Si Kweli
10. O Si Kweli
11. O Si Kweli
12. X Kweli
13. O Si Kweli
14. O Si Kweli
15. X Kweli
16. O Si Kweli

### Ukurasa wa 2

17. X Kweli
18. X Kweli
19. X Kweli

**Maswali ya Kuchagua Kati ya Majibu Mengi** (Alama 2 kwa kila moja)

1. B
2. C
3. B
4. B

# Kanuni ya Kikristo
## Mtihani wa 1: Toleo la 5,
## Karatasi Ya Majibu Kwa Ajili Ya Mwalimu

### Ukurasa wa 3

**Kulinganisha** (Alama 3 kwa kila moja)

1. B

2. D

3. E

4. A

5. F

6. C

### Maswali ya Majibu Mafupi

1. Alama 5

   Mwili wa Kristo

2. Alama 5

   Damu ya Yesu

3. Alama 24

   Waefeso 4:29, 2 Wakorintho 9:7, Wakolosai 3:23

### Ukurasa wa 4

4. Alama 21

   Jibu lako binafsi

# Kanuni za Kikristo
## Mtinani Simulizi wa 2 Toleo la 5

### Maagizo

Andika majibu yako kwa karatasi nyingine uliyopewa. *Usiandike* kwa karatasi hii ya mtihani. Yafanye majibu yako kueleweka vizuri kabisa. Andika kwa njia maalum (iliyo bayana). Baadhi ya maswali yanataja ni sehemu ngapi au ni majibu mangapi tofauti unayopaswa kuandika ili kupokea alama zote katika swali hili. Baadhi ya maswali yana swali lingine katika mabano. Hili ni swali lilo hilo ila tu kwa maneno tofauti.

### Maswali

1. Ni nini kusudi la ubatizo wa maji?
   (Mbona ubatizwe kwa maji?) (Alama 10)

2. Unapohusika katika ibada ya Ushirika Mtakatifu, ni mambo gani unayopaswa kutafakari? (Ni kwa nini tuwe na ibada ya Ushirika Mtakatifu?)
   Jibu lenye sehemu 5. (Alama 3 kwa kila sehemu)

3. Ni vipi unakuwamenejawa Mungu? (alama 5)

4. Orodhesha vitu vitatu ambavyo Mungu amekupa ili usimamie. Eleza jinsi unavyoweza kuwa meneja mzuri wa kila mojawapo ya vitu hivi, na jinsi kutenda hivyo kutakavyoathiri maisha yako.
   Jibu la sehemu 3. (Kila moja alama 5 kwa kila jibu lililokamilishwa)

5. Kwa nini tuwe na kanisa la mahali pamoja?
   (Ni yapi malengo mawili ya umbali ya kanisa la mahali pamoja?
   Jibu lenye sehemu 2. (alama 5 kwa kila sehemu)

6. Katika darasa tulijadili kile mtu anaweza kufanya ili kufurahia kuwa sehemu ya kanisa la mahali pamoja. Kuna miongozo minne mikuu au kanuni zinazofanya kanisa liwe na afya. Taja miongozo hii mitatu. (alama 4 kwa kila sehemu)

7. Andika ushuhuda wako ukitumia miongozo uliopewa darasani.
   Onyesha jinsi ulivyoweza kutumia andiko kukusaidia hasa katika sehemu moja kwa maisha yako ya kila siku. (Alama 12)

8. Toa mfano maalum wa ombi moja ambalo Mungu umekujibu ndani ya wiki iliyopita.
   (Alama 5)

9. Andika mistari ya kukariri. (alama 12, kila mstari alama 4)

# Kanuni za Kikristo

## Mtihani wa 2, Mtihani wa Simulizi, Toleo la 5
## Karatasi Ya Majibu Kwa Ajili Ya Mwalimu

**Andiko la Mwalimu:** Majibu yanapaswa kuandikwa kwa karatasi tofauti na hii. Majibu yaliyopendekezwa ambayo yameorodheshwa hapa chini yameandikwa tu kwa muhtasari. Huenda utawataka wanafunzi kuandika zaidi ya kile kimeorodheshwa hapa chini.

**1. Ni nini kusudi la ubatizo wa maji?**
**(Mbona ubatizwe katika maji?) (Alama 10)**

Kumtii Mungu

Ni ushuhuda wa hadharani kwamba nifanyika kuwa Mkristo.

Ni hatua nyingine katika kukua kwangu kiroho

**2. Unapohusika katika ibada ya Ushirika Mtakatifu, ni mambo gani unayopaswa kutafakari? (Ni kwa nini tuwe na ibada ya Ushirika Mtakatifu?)**
Jibu lenye sehemu 5. (Alama 3 kwa kila sehemu)

Majibu Yaliyopendekezwa

1. Kumwabudu Mungu.
2. Kukumbuka kuwa Yesu ulitufia.
3. Kumtamia ujio wa Yesu wa mara nyingine.
4. Tazama ndani yako ili kuchunguza maisha yako.
   a. Omba Mungu akusamehe dhambi zako.
   b. Angalia kama umefikia malengo yako.
5. Tazama uhusiano wako na wengine.
   a. Omba msamaha.
   b. Mtie mtu moyo.
   c. Mshukuru mtu kwa kile alichokitenda.

**3. Ni vipi unakuwamenejawa Mungu? (alama 5)**

Majibu yaliyopendekezwa

-Kutoa maisha yako kwa Kristo

-Kwa kuwa mwaminifu

# Kanuni za Kikristo
## Mtihani wa 2, Mtihani wa Simulizi, Toleo la 5
## Karatasi Ya Majibu Kwa Ajili Ya Mwalimu

**4. Orodhesha vitu vitatu ambavyo Mungu amekupa ili usimamie.**

**leza jinsi unavyoweza kuwa meneja mzuri wa kila mojawapo ya vitu hivi, na jinsi kutenda hivyo kutakavyoathiri maisha yako.**

Jibu la sehemu 3. (Kila moja alama 5 kwa kila jibu lililokamilishwa)

Majibu yaliyopendekezwa hapa chini ni ya sehemu ya kwanza tu ya swali hilo. Ni lazima waeleze sehemu nyingine ya jawabu lao kama ilivyoelekezwa katika swali ili kupata alama zote.

1. Wakati
2. Fedha
3. Karama za Roho Mtakatifu
4. Familia
5. Kazi

**5. Kwa nini tuwe na kanisa la mahali pamoja?**

**(Ni yapi malengo mawili ya umbali ya kanisa la mahali pamoja?)**
Jibu lenye sehemu 2. (alama 5 kwa kila sehemu)

1. Kuwasaidia Wakristo kuwa na nguvu kiroho.
2. Kushiriki Kristo na wale wasio Wakristo.

**6. Katika darasa tulijadili kile mtu anaweza kufanya ili kufurahia kuwa sehemu ya kanisa la mahali pamoja. Kuna miongozo minne mikuu au kanuni zinazofanya kanisa liwe na afya. Taja miongozo hii mitatu.**
(Alama 12, alama 4 kwa kila sehemu)

Majibu Yaliyopendekezwa

1. Watu wanapaswa kujumuika pamoja kwa ajili ya ushirika.
2. Watu wanapaswa kujumuika pamoja kuabudu Mungu na kuomba.
3. Watu wanapaswa kujumuika pamojakumsikiliza Mungu.
4. Watu wanapaswa kujumuika pamoja ili kusaidiana wao wenyewe.

# Kanuni za Kikristo

## Mtihani wa 2, Mtihani wa Simulizi, Toleo la 5
## Karatasi Ya Majibu Kwa Ajili Ya Mwalimu

**7.** **Andika ushuhuda wako ukitumia miongozo uliopewa darasani.**
**Onyesha jinsi ulivyoweza kutumia andiko kukusaidia hasa katika sehemu moja kwa maisha yako ya kila siku.**

(Alama 16, kila sehemu alama 4)

**Andiko la Mwalimu:** Ushuhuda wa mwanafunzi unapaswa kujumuisha miongozo minne iliyotumika katika kozi hii.

Hii hapa ni miongozo hiyo:

1. Eleza eneo moja katika maisha yako ya kila siku pale ambapo Mungu anakusaidia kukua.
2. Taja mstari mmoja katika Biblia ambao umekusaidia kukua katika eneo hili la maisha yako. Ikiwa umekariri aya hiyo, basi inukuu. Au soma kutoka kwa Biblia yako.
3. Eleza jinsi umeutumia mstari huu kukusaidia katika eneo hili moja la maisha yako. Usihubiri. Eleza kwa njia rahisi na inayofaa jinsi aya hii inakusaidia. Eleza jinsi aya hii inahusiana na eneo la maisha yako ambapo Mungu anakusaidia kukua.
4. Toa mfano mmoja maalum kutoka siku chache zilizopita kuonyesha jinsi ulivyotumia aya hii. Mpe Mungu sifa kwa kukusaidia kukua.

**8.** **Toa mfano maalum wa ombi moja ambalo Mungu umekujibu ndani ya wiki iliyopita.**

(Alama 5)

Jibu la mtu binafsi.
Tumia tathmini yako mwenyewe kutoa alama kutokana na majibu yao kwa swali hili.

**9.** **Andika mistari ya kukariri.** (Alama 12, kila mstari alama 4)

Waefeso 4:29, 2 Wakorintho 9:7, Wakolosai 3:23

## Hongera

______________________________

Amemaliza

# Kanuni za Kikristo

Tunatambua kujitoa kwako katika masomo haya na ni matumaini yetu kwamba kwa mafanikio utaendelea na masomo yako yajayo.

Wakufunzi ______________________

Tarehe ______________________


## Hongera

______________________________

Amemaliza

# Kanuni za Kikristo

Tunatambua kujitoa kwako katika masomo haya na ni matumaini yetu kwamba kwa mafanikio utaendelea na masomo yako yajayo.

Wakufunzi ______________________

Tarehe ______________________